# Nipashe

Jumamosi Juni 17, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581344

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

## Utafiti wabaini tatizo kijinsia katika vyombo vya habari

UKURASA 4




## CCM yamulika utatuzi kero 3 bajeti 2023/24


UKURASA 5


Prof. Humphrey Moshi

### TOZO MPYA MAFUTA, SARUJI

# Wachumi waipa angalizo serikali

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Kamishna wa Polisi Benedict Wakulyamba kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Hofu upigaji yatanda, CAG aamua kufanya uchunguzi zaidi

UKURASA 15



# Siri uteuzi kina Lukuvi Ikulu

• **Samia** aweka wazi, ataja sababu kutumbua vigogo wa RITA... *Ukurasa 2*

**MICHEZO** IBENGE ATAJWA KUMRITHI NABI YANGA UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6


# Samia aweka wazi sababu uteuzi Lukuvi, vigogo RITA



William Lukuvi



Abdallah Bulembo



George Mkuchika

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaja sababu za kuteua viongozi wapya, akiwamo anayekwenda kushughulika na shida za kiutendaji zinazolikabili Jeshi la Uhifadhi, na kuwapa hadhi ya ubalozi baadhi ya viongozi katika ofisi yake.

Pia amesema ameteua mavetenari wanne wakiwamo aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi na Abdallah Bulembo kuwa washauri wa Rais (Siasa na Uhusiano wa Jamii) ili kusaidiana na Kapteni mstaafu George Mkuchika na hivi karibuni watakwenda ngazi za chini kuibua kinachokosekana, jamii ikoje na siasa na kutoa mapendekezo kwake.

Akizungumza jana Ikulu Chamwino, Dodoma baada ya kuwaapisha wateule hao, Rais Samia aliweka bayana sababu za kufanya uteuzi wa viongozi hao zikijumuisha ukuaji wa nchi baada ya kuifungua na sasa inakuja na mambo mengi, hivyo wasaidizi ni lazima wawe wengi zaidi.

Pia alisema kuna ongezeko la watu ambao wanahitaji huduma, hivyo lazima wahakikishe kila sekta kuna waliozishika ili kutoa huduma kwa wananchi.

"Tunafanya mabadiliko kwa sababu hiyo, hivyo wale mnaoteuliwa nendeni kafanyeni hayo, nendeni kafanyeni kazi," aliagiza.

**JESHI UHIFADHI**

Akitaja sababu za kila mteule aliyemwapisha, Rais Samia alisema amemteua Kamishna Benedict Wakulyamba kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utalii na Maliasili kwa sababu moja kubwa - kwenda kusimamia changamoto wanazozisikia kila siku katika Jeshi la Uhifadhi.

"Kila siku tunasikia kesi za Jeshi Usu - mara wameingiza nani, mara wameuana, mara wameuliwa, mara sijui hifadhi imefanyaje. Kuna mambo mengi sana huko Jeshi Usu. Sasa wewe ni mwanajeshi mwenzao, nenda kasimamie nidhamu ya Jeshi Usu.

"Hiyo ndio kazi yako mahususi kusimamia hifadhi zetu na majeshi yetu, jeshi letu lile linavyokwenda kuzisimamia hifadhi zetu. Kwa hiyo, ndiyo kazi yako mahususi na zile ambazo atakazokupangia waziri wako au katibu mkuu wako," alielekeza.

**WASHAURI SIASA**

Rais Samia alisema amewateua 'magwengwe' wanne, Lukuvi, Bulembo, Haji Omar Kheir na Balozi Rajab Omar Luhwavi kwa kuwa wanakokwenda wana kazi kubwa ya kuoanisha siasa na maendeleo ya jamii.

"Siasa tumekiachia chama moja kwa moja lakini kule kwenye chama kuna nenda rudi, vuta, purura, sukuma. Kama mnavyojua niliteua waziri ndani ya Ofisi ya Rais mwenye kazi maalum; kaka yetu Mkuchika.

"Sasa hii ndio kazi yake maalum. Peke yake asingeweza kufanya. Kwa hiyo, nimemteulia mavetenari wenziwe hao waende wazame huko chini watuambie nini kinakosekana.

"Jamii ikoje na siasa? Siasa zetu nchini zinakwendaje? Mambo yakoje? Waende wakatutafutie huko, watuambie na waje na mapendekezo - nini tufanye ili watanzania wote wawe ndani wanapokwenda na maendeleo ya jamii ndani ya nchi yetu?

"Hiyo ndiyo kazi kubwa ya washauri hawa na watafanya kazi Tanzania nzima," Rais Samia alifafanua.

Alisema kuwa chini ya uongozi wa waziri wao, hivi karibuni watakwenda kujipangia na kupangiwa kazi zao na kuanza kazi.

**TAMISEMI**

Kuhusu Rogatus Hussein Mattivila, Rais Samia alisema alifanya vizuri akiwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), hivyo amemteua kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Miundombinu) ili akasimamie eneo hilo.

"Lazima tuwe na mtu maalum wa miundombinu na nikahisi Injinia Mativila anakwenda kutufaa huko, atakwenda kusimamia miundombinu yote itakayojengwa ya nchi hii ndani ya TAMISEMI, wapi hakujakaa sawa, wapi kuna kasoro hizi.

"Atakwenda kuzishughulikia na kuhakikisha miundombinu inayojengwa ni ya thamani ya fedha tunazopeleka. Fedha nyingi zinakwenda huko lakini hazina usimamizi mzuri," alisema Rais Samia.

**HADHI UBALOZI**

Rais Samia pia alisema amempandisha hadhi ya ubalozi, Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Kusiluka, kwa kuwa ni msaidizi wa karibu zaidi na Rais.

"Kuna nyakati Rais anazongwa na kazi nyingi, na kuna wageni wanaotaka kumwona Rais ambao mtu asiye na hadhi ya ubalozi wanakuwa wanyonge kumwona. Kwa hiyo, tumempa hadhi Katibu Mkuu Kiongozi, ili apate upeo mpana wa kufanya kazi zake akutane na wengi zaidi, anipunguzie mimi mzigo huku.

"Kwa sababu sasa hivi nikitoka kuna wageni wananisubiri. Sasa yeye angekuwa na ule uzito ningemwambia wapelekeni kwa Katibu Mkuu Kiongozi, tumempa kazi hiyo ili aweze kufanya hiyo kazi. Lakini huwezi kujua huko mbele..." alitoa angalizo.

Akimwelezea Balozi Salim Othman Hamad, Msaidizi wa Rais anayeshughulikia siasa, Rais Samia alisema wamempa hadhi hiyo kwa sababu mambo ya siasa hayako tu katika vyama.

Mkuu wa Nchi alisema hata katika balozi zilizopo nchini siasa ipo zinazoitwa 'mazungumzo ya kisiasa' ambayo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki hufanya.

"Tumependa wakati wanafanya hivyo, Balozi Salim awe anashiriki kule ili ofisi yangu iwe imeshiriki moja kwa moja ili tujue kitu gani tuchukue hatua haraka, kimesemwa nini? Lakini na yeye huwezi kujua, mbele huko tunaweza kumtafutia kituo," alisema.

Kwa upande wa Balozi mteule Dk. Kassim Mohamed Khamis, Msaidizi wa Rais anayeshughulikia hotuba, Rais Samia alisema "kwa umri wake atabaki nchi kavu".

Alisema amefanya kazi kwa muda mrefu Umoja wa Afrika (AU) akiwa mchambuzi wa mambo mengi ya AU, akiandika majarida mengi.

"Tumeona tukamilishie cheo chake, tumpe ubalozi ili akamilike, lakini yeye anabaki kuwa wa nchi kavu hapa, ataendelea kufanya uchambuzi ndani ya ofisi yangu," alisema.

Rais Samia pia alimtaja Balozi Idd Seif Bakari, alikuwa Dubai kama Mkuu wa Kituo cha Dubai na sasa anakwenda Uturuki.

**VIGOGO RITA**

Kuhusu uteuzi wa viongozi wapya wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Rais alisema Kabidhi Nasihi Mkuu mpya na naibu wake amewateua baada ya kuwaondoa waliokuwapo. "Nilikuwa ninategemea watu wapate huduma ndani ya ile ofisi huduma za kuridhisha kabisa, kilichokuwa kinatokea mule ndani ni ugomvi.

"Labda nilikuwa ninasema wote ni kina mama ndio maana kulikuwa na ugomvi mkubwa lakini ukiangalia kwa ndani kulikuwa kuna kutokutekelezeka kwa kazi vizuri, mwingine akisema mwingine anakasirika, mwingine akirekebisha mwingine anachafua.

"Nikaamua kuwaweka wote upande wa pili wapangiwe kazi nyingine. Sasa nendeni ninyi wawili, ninataka mkashirikiane mkatoe huduma kwa wananchi, ile ni ofisi kubwa wananchi wanaitegemea.

"Badala ya kujenga 'maugomvi' huko ndani, nendeni kashirikianeni, angalieni wapi kumeharibika wekeni sawa.

"Kuna kesi zinakuja kwetu mkiwaambia 'hebu rudini piteni njia zinazohusika', wanasema 'kule hakuendeki', hatujui kinachoendelea. Kwa hiyo, ili wananchi wapate huduma vizuri, nendeni kakaeni mkafanye kazi," alisema.

Juni 11 mwaka huu, Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu ilitangaza kuwa Rais Samia amemteua Frank Kanyusi kuwa Kabidhi Wasihi Mkuu. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mwanasheria Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara.

Taarifa hiyo ya Ikulu pia ilibainisha kuwa Rais amemteua Irene Lesulie kuwa Naibu Kabidhi Wasihi Mkuu. Kabla ya utuezi huo, alikuwa Mkurugenzi Msaidizi (Mshauri ya Kimataifa) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

# Wachumi watoa angalizo kwa serikali tozo mafuta, saruji

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

SIKU moja baada ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuwasilisha mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, akipendekeza kuwapo ongezeko ushuru na tozo katika saruji na mafuta (petroli na dizeli), wachumi waipa angalizo serikali kuhusiana na pendekezo hilo.

Akiwasilisha juzi bungeni jijini hapa mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/24, Waziri Mwigulu alisema anapendekeza kuongeza ushuru katika saruji.

Waziri alisema serikali inapendekeza kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha Sh. 20 kwa kila kilo ya sarufi inayotoka nje ya nchi na inayozalishwa ndani ya nchi. Hii ina maana kwamba serikali itapata Sh. 1,000 kwa kila mfuko wa kilo 50 kupitia tozo hiyo mpya.

Pia alisema serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220, kwa kuongeza ushuru wa barabara na mafuta kwa Sh. 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli.

Alisema lengo la tozo hizo ni kupata fedha ambazo zitaelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Makadirio ni kupata Sh. bilioni 381.8 kwa mwaka huo wa fedha.

Katika mazungumzo na Nipashe jana kuhusu mapendekezo hayo ya bajeti ya serikali, baadhi ya wachumi walionya kuwa ongezeko hilo litachochea mfumuko wa bei.

Profesa wa Uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Hamphrey Moshi, alisema tozo hizo katika mafuta na saruji zitachochea mfumuko wa bei na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi.

Alisema mafuta yanapopanda bei, hugusa kila kitu na kusababisha nauli na gharama za usafirishaji wa mizigo kupanda kwa kuwa karibu kila kitu hutegemea usafiri, hivyo hata bei za vyakula nazo zitapanda.

Kuhusu saruji, Prof. Moshi alisema tozo mpya itasababisha mfumuko wa bei kwa vifaa vya ujenzi. Alitolea mfano, kwa sasa kuna mfumuko wa bei ambao umetokana na vita vinavyoendelea vya Russia na Ukraine pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

"Kwa mfano, Tanzania tunategemea ngano, mafuta ya kula na mbolea toka nchi za nje. Vyote vinasafirishwa kuja Tanzania. Kwa hiyo, ongezeko la bei ya mafuta litachangia sana kupanda kwa gharama za bidhaa.

"Kitu ambacho ninaishauri serikali ni kuendelea kuhakikisha bei ya dizeli inakuwa chini ya petroli....," alisema Prof. Moshi.

Kuhusu uamuzi wa serikali wa kuondoa ada katika vyuo vya kati, mchumi huyo alisema ni wa kupongezwa kwa kuwa vilikuwa vinaelekea kufa. Uamuzi utaongeza wasomi watakaoishi hata nje ya mfumo wa ajira.

Mchumi mwingine kutoka Taasisi ya Usimamizi Wajasiriamali na Maendeleo (IMED), Dk. Donath Olomi, alisema kuongeza tozo katika saruji kutapandisha bei ya bidhaa hiyo, hivyo kutaongeza gharama za ujenzi.

Alisema athari zitaonekana katika utekelezaji wa miradi ya sekta mbalimbali ikiwamo shuleni na hata miradi mikubwa ya serikali.

Akitoa maoni yake kuhusu pendekezo la kufuta ada katika vyuo vya kati, Dk. Olomi aliutaja ni uamuzi mzuri kwa kuwa serikali inaandaa mtaala ambao utahitaji walimu wengi wa ufundi.

"Ni hatua nzuri, itawapa vijana nafasi ya kusoma katika vyuo vya kati bila kikwazo. Ilifika mahali watu waliamini ufundi haulipi, wanafunzi walikuwa wanakwenda kusomea sheria na ualimu lakini hatua hii itasaidia kupata walimu wengi na wahitimu wanaoweza kujiajiri," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), Dk. Paul Loisulie, alisema bajeti hiyo imelenga kumfikia na kumnyanyua mtu wa chini. Awe sehemu ya maendeleo ya nchi.

**WABUNGE**

Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali (CCM), alisema bajeti hiyo italeta ahueni kwa wafanyabiashara kutokana na kusudio la kupunguziwa mzigo wa kodi ikiwamo Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Aliitaja ni bajeti itakayowapunguzia mzigo watanzania wa hali ya chini kutokana na kuondolewa ada katika vyuo vya kati na kuongeza fursa ya kupata elimu ya ufundi kwa vijana na kuwa sehemu ya maendeleo ya nchi.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa, Ritta Kabati (CCM), alisema bajeti pendekezwa imeonyesha kumjali mwananchi wa hali ya chini.

Ritta alisema bajeti hiyo itakwenda kuongeza wasomi ambao watakuja kuendesha miradi ya maendeleo na kuchangia kukuza uchumi kwa kuwapa mikopo wanafunzi waliomaliza kidato cha nne na kuchaguliwa na serikali kusoma vyuo vya ufundi.

Pia alisema ni bajeti itakayoleta suluhisho kwenye miundombinu mibovu ya barabara na sekta ya kilimo, hasa katika maeneo ya vijijini.

Mbunge wa Chumbuni visiwani Zanzibar, Ussi Salum Pondeza, alisema bajeti pendekezwa imeondoa ugomvi uliokuwapo wa muda mrefu kati ya wafanyabiashara na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kupunguza kodi.

"Ni bajeti ya kutofunga biashara zao na kurekebisha uchukuaji wa kodi za mizigo bandarini kwa kumpa nafasi mfanyabiashara aliyeshindwa kulipa kodi hiyo kuchukua mzigo wake na kuendelea kulipa akiwa anauza," alisema.

Mbunge wa Hai, Saashisha Mafuwe, aliitaja ni bajeti yenye unafuu kwa wananchi huku akimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anakuja na miradi inayoleta unafuu kwa wananchi.

# Polisi walivyoua watatu wakidaiwa majambazi

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

JESHI la Polisi mkoani Geita limeua watu watatu wanaodaiwa majambazi katika tukio linalotajwa la majibizano ya risasi kati ya askari polisi na watuhumiwa hao.

Katika tukio hilo, Jeshi la Polisi limedai kupata silaha aina ya Mark IV inayodaiwa kuporwa kwa mlinzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi wa Polisi Safia Jongo, alisema tukio hilo lilitokea Juni 12 jioni baada ya watuhumiwa hao kudaiwa kuvamia vibanda sita vya wafanyabiashara katika Kijiji cha Kasota wilayani Geita.

Alisema kuwa wakati askari wanaendelea na operesheni na watu hao kukaidi amri ya polisi ya kujisalimisha, kulitokea majibizano kati yao na kusababisha vifo hivyo.

Kamanda huyo alisema watuhumiwa hao wanakadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 30 hadi 40. Wamo wanaodaiwa kujihusisha na matukio ya uvamizi wa maduka na vibanda mkoani na walikuwa wanasakwa na jeshi hilo.

Kamanda huyo alitaja matukio mengine ambayo watuhumiwa hao wanadaiwa kuyafanya ni uvamizi wa vibanda vya wafanyabiashara katika Kijiji cha Ntinachi Aprili 23 mwaka huu na kupora Sh. milioni 31.2 na lingine la Mei 23 mwaka huu eneo la Njiapanda ya Inyara, Katoro, wakidaiwa kupora Sh. milioni 17.3.

Kamanda Jongo alisema operesheni ya kuwasaka watuhumiwa wote waliohusika na matukio ya uhalifu inaendelea huku akiwataka viongozi wa serikali za mitaa na watendaji kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi ili kukabiliana nao.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**
**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

eGA

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mkuu**

**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"



Mratibu wa Shirika la Msaada wa kisheria wilayani Liwale mkoani Lindi, (LIWOPAU), Hidaya Chikawe, akitoa elimu ya mambo ya sheria kwa wakazi Kijiji cha Mtawango, Kata ya Mbaya wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Ripoti mpya yabaini tatizo kijinsia vyombo vya habari

**Na Enock Charles**

RIPOTI mpya kuhusu hali ya usalama wa waandishi wa habari kwa kuzingatia jinsia, imebaini asilimia 72 ya wanawake katika vyombo vya habari hufanya kazi za kawaida zisizoendana na uandishi wa habari kama vile usafi, mauzo na kutafuta masoko.

Kutokana na hali hiyo, wito umetolewa kwa vyombo vya habari kuweka mifumo ya kupambana na ukatili wa kijinsia na kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za habari.

Hayo yamebainishwa katika ripoti ya utafiti huo iliyotolewa juzi Dar es Salaam na Mratibu wa Tathmini na Ufuatiliaji kutoka shirika lisilo la kiserikali la Africa Freedom of Information Centre (AFIC), Charity Komujjurizi.

Alisema kuwa utafiti huo uliofanywa kwa miaka mitano (2016-2021), umebaini kuwa hata wanawake wanaofanikiwa kufanya kazi ya uandishi wa habari nchini, hawapewi majukumu makubwa na motisha mbalimbali kama ilivyo kwa wanaume.

Ni hali ambayo Komujjurizi anaitaja inawarudisha nyuma maendeleo ya wanawake katika fani hiyo na kiuchumi.

"Utafiti unaonyesha wanawake wanaofanya kazi katika vyombo vya habari ni asilimia 40 lakini ni asilimia 28 tu wanaofanya kazi za habari.

"Asilimia 72 wanafanya kazi za kiutawala, usafi, mauzo, masoko, huduma za vyakula na usambazaji," alinukuu sehemu ya ripoti ya utafiti huo.

Alisema utafiti huo pia umebaini ni asilimia 21 ya wanawake katika vyombo hivyo ambao wapo katika uongozi na asilimia 20 katika uongozi wa juu huku akipatikana Mkurugenzi Mtendaji mmoja katika vyombo 50 vya kielektroniki.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kazi wanazopewa waandishi wa habari wanawake ni za kutafuta habari za kawaida hasa zinazohusu burudani na masuala ya kifamilia tofauti na waandishi wanaume ambao hupewa jukumu la kutafuta habari ngumu hasa kuhusu siasa na uchumi.

Ripoti inabainisha kuwa wanawake wanawake pia hupewa ujira mdogo kulinganishwa na wanaume.

Meneja wa Mipango na Mikakati kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Slyvia Daulinge, aliwataka wanawake wanaonyanyaswa katika vyombo vya habari kujitokeza kusema yale yanayowasibu na kuacha unyonge ili wapate msaada kutoka katika jamii inayowazunguka na taasisi mbalimbali.

"Uzoefu unaonyesha kwamba wanawake wanahabari wanafanyiwa ukatili ndani ya vyombo vya habari na viongozi wao wakubwa ndani ya vyombo vya habari, lakini wanaigiza kama kila kitu kipo sawa tu. Wanapofanya kazi zao za kila siku," alisema.

Aliongeza kuwa TAMWA ina mikakati ya kuwajenga uwezo wanawake wa aina hiyo ili wapaze sauti zao na kuwa mfano kwa wengine kwa kuwa zipo taasisi nyingi za kuwasaidia kutatua changamoto zao.

Aliwataka wazitumie taasisi hizo zinazojumuisha TAMWA yenyewe, Baraza la Habari Tanzania (MCT), MISA Tanzania na Klabu ya Waandishi wa Habari Tanzania.

Akizungumza katika uzinduzi wa ripoti hiyo, Mkurugenzi wa Uchechemuzi kutoka Twaweza, Risha Chande, alisema pamoja na uhitaji uliopo wa marekebisho ya sheria mbalimbali ili kupambana na ukatili wa kijinsia, anaamini hata sheria zilizopo zikitumiwa vizuri, zinatosha kupambana na ukatili huo kama itatolewa elimu katika jamii.

"Mimi sioni kama utatuzi wa hili tatizo ni kwenye sera na kanuni. Masuala kama ya unyanyasaji wa mtandaoni hatuwezi kuwa na polisi kila siku kwenda kusoma mtandaoni, tunahitaji kuelimishana na kusemana sisi wenyewe," alisema Risha.

# Mwongozo usimamizi miundombinu iliyoko ardhini wazinduliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWONGOZO wa usimamizi wa pamoja wa miundombinu iliyoko chini ya ardhi katika njia zinazotumiwa na taasisi na kampuni za huduma, umezinduliwa, ukilenga kudhibiti ongezeko la shughuli zisizoratibiwa chini ya ardhi zinazosababisha athari kubwa za kiusalama, uharibifu wa mali, mazingira na ajali kwa watu.

Uzinduzi huo ulifanywa jana jijini hapa na Kamishna wa Petroli na Gesi wa Wizara ya Nishati, Michael Mjinja, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Felchesmi Mramba.

Akizungumza katika uzinduzi wa mwongozo huo ulioandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mjinja aliagiza wamiliki na watumiaji wake kuufuata wanapotekeleza majukumu yao. Mjinja alisema mwongozo huo una lengo la kuimarisha usalama wa umma, kuongeza uadilifu na usimamizi makini wa miundombinu iliyopo chini ya ardhi Tanzania Bara.

"Mwongozo huu utasaidia katika kuratibu shughuli za ujenzi, uendeshaji, marekebisho na matumizi mengineyo ya mikuza inayotumiwa kwa pamoja na wadau mbalimbali bila kuathiri usalama wa miundombinu, umma na mali zao," alisema.

Akizungumzia chimbuko na utaratibu wa utengenezaji mwongozo huo, Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Timu ya Watalaamu JSC, DK. Michael Mngodo, alisema kumekuwa na ongezeko la shughuli zisizoratibiwa kwa pamoja katika utaratibu usio rasmi kwa miundombinu iliyoko chini ya ardhi. Aliitaja ni hali inayosababisha athari kubwa za kiusalama, uharibifu wa mali mazingira na ajali kwa watu.

"Mfano ni ajali za kupasuliwa kwa mabomba ya gesi asilia, mafuta na maji wakati wa shughuli za ujenzi na maboresho ya miundombinu katika maeneo mbalimbali.

"Mifano ya ajali kama hizi ipo mingi hasa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayohusisha uchimbaji wa ardhi," alisema. Mkurugenzi Mkuu EWURA, James Andilile, alisema shughuli za uchimbaji ili kutandaza miundombinu katika mikuza (njia) haziepukiki kwa kuwa mahitaji ya huduma zinazotolewa na kampuni mbalimbali zinazidi kuongezeka na kufanyika bila ya kuratibiwa.

"Kwa usalama wa miundombinu iliyoko chini ya ardhi, tunaamini wamiliki na watumiaji, wataufuata mwongozo huu katika utumiaji wa mikuza ili kulinda miundombinu hiyo, kuepusha migogoro na kuokoa maisha ya watu na mali zao,"alisema.

# RC ataka DED aanze na watumishi 'mizigo'

**Na Moses Ng'wat,** ILEJE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Dk. Fransis Michael, amemtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ileje, Nuru Kindamba, kuchukulia hatua dhidi ya watumishi watakaoonekana kukwamisha kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri hiyo.

Alitoa agizo hilo jana katika kikao cha Baraza Maalum la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichoitishwa kwa ajili ya kupitia na kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2021/22. Halmashauri hiyo imepata hati safi.

Dk. Francis alitoa kauli hiyo baada ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Songwe, Radwel Mwampashi, kuwalalamikia baadhi ya watumishi kutowajibika ipasavyo katika majukumu yao, akiitaja ni hali inayochangiwa na watumishi hao kukaa muda mrefu katika halmashauri hiyo.

Kufuatia malalamiko hayo, Mkuu wa Mkoa alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ileje, Kindamba, ambaye hivi karibuni aliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha anachukua hatua kali kwa watumishi wataoonekana kuwa kikwazo.

"Mkurugenzi ninadhani umesikia mwenyekiti wa chama alichosema. Kama kuna mtumishi ataonekana kikwazo katika kutekeleza majukumu yako au kukuyumbisha ili usifikie malengo, wewe wasilisha jina lake ofisini kwangu ili tuchukue hatua za kisheria.

"Tukibaini mtumishi anafanya kwa uzembe, tutamchukulia hatua na kama liko ndani ya uwezo wa mtumishi basi tutamwezesha," alionya.

Alisema kumekuwa na shida katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, hasa katika ukamilishaji wa miradi ya maendeleo licha ya serikali kupeleka fedha nyingi.

Mkuu wa Mkoa pia alilitaka Baraza la Madiwani kuchukua hatua dhidi ya watumishi wazembe, lakini kusiwe na anayeonewa.

Awali Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Songwe, Mwampashi, alilalamikiaa baadhi ya watumishi kutowajibika ipasavyo katika utekelezaji wa majukumu yao na kumtaka Mkurugenzi Mtendaji huyo mpya na uongozi wa mkoa kuchukua hatua dhidi yao.

Alisema uzembe wa baadhi ya watumishi katika halmashauri hiyo umechangiwa na wengi wao kukaa kwa muda mrefu katika kituo cha kazi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ileje, Ubatizo Songa, alisema baraza lake liko tayari kuyasimamia maelekezo yote na kuwawajibisha watumishi wazembe ili miradi ya maendeleo iende kwa kasi na kupunguza adha kwa wananchi.

HABARI KITAIFA

# CCM yaona utatuzi kero tatu bajeti ya serikali

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA.

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ametaja mambo matatu yaliyokuwa kilio kwa wananchi na sasa yatatatuliwa kupitia bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/24.

Chongolo aliyataja mambo hayo jana katika Kata ya Kingiti wilayani Mpwapwa katika mfululizo wa ziara zake mkoani Dodoma.

Alisema amri ya kufungi abiashara za watu kabla ya kufanya nao majadiliano ilisababisha serikali kupata hasara na wafanyabiashara wenyewe.

Aliitaja kero ya pili itakayoondolewa kupitia bajeti hiyo ni kuweka programu ya mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya kati, jambo ambalo litasaidia kuongeza mafundi wenye ujuzi.

Chongolo alisema jambo la tatu ni kufufuliwa kwa viwanda ambavyo vitaongeza ajira kwa vijana wengi nchini.

Wakati wa kuwasilisha mapendekezi ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alitangaza kupiga marufuku utaratibu wa kufunga biashara kwa anayedaiwa kodi.

Dk. Mwigulu pia alisema serikali kuanzia mwaka ujao wa masomo, itakuwa na programu ya mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya kati wanaochukua masomo ya sayansi, ufundi, afya na ualimu.

Katibu Mkuu Chongolo alisema kufunga biashara kulisababisha watu kujenga chuki na serikali yao kwa kuwa kumfungia mtu biashara yake kisha unaendelea kumdai, ni kupoteza muda. Atapata wapi fedha za kukulipa?

Alisema mikopo ya vyuo vya kati inakwenda kuinua uchumi wa Taifa na kuongeza ajira kwa vijana wengi kwa kuwa kundi hilo likikosa fursa za kusoma vyuoni kutokana na kukosa mikopo.

Katibu Mkuu pia aliwataka wasimamizi wa mamlaka za maji nchini kupima na kuviwekea uzio vyanzo vya ili kuepuka uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo hivyo.

Chongolo alisema zamani maeneo mengi nchini yalikuwa na maji mengi yaliyotiririka msimu wote lakini watendaji wameshindwa kuwazuia watu kuvivamia vyanzo vya maji na kusababisha uharibifu wa vyanzo hivyo.

Mwenyekiti wa Shina Namba Nane ambako walifanyia mkutano huo, Daniel Msihi, alimwambia Katibu Mkuu kuwa ukosefu wa maji unatokana na uharibifu mkubwa wa mazingiria kijijini huko.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema Jimbo la Kibakwe wilayani Mpwapwa linakabiliwa na uhaba wa maji ingawa kuna miradi inayoendelea huko.



MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akizungumza jana na wananchi wa vijiji vya Ishinsi, Ndurumo, Msingi na Kidi kata ya Msingi wilayani Mkalama wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa mradi skimu ya umwagiliaji ya Msingi. Ujenzi wa mradi huo unaanza mwezi huu. **PICHA : THOBIAS MWANAKATWE**

# UNCDF yanasa dawa mabadiliko tabianchi

**Na Restuta James**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (UNCDF) limesema upatikanaji wa uhakika wa gesi, mafuta maalum ya kupikia (bioethanol), mkaa na kuni mbadala ndilo suluhisho la uharibifu wa mazingira utakaopunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ofisa Mwandamizi wa Masuala ya Fedha wa UNCDF ambaye pia ni Meneja wa Mradi wa Cookfund, Imanuel Muro, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipozindua kampeni ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ya 'Anzia Jikoni-mabadiliko ya hewa safi ya baadaye yanaanzia jikoni'.

Alisema ili kuwezesha upatikanaji wa nishati safi, Umoja wa Ulaya (EU), umetenga EURO milioni 17 (takribani Sh. bilioni 47.6), kwa ajili ya kufadhili kampuni na wajasiriamali wanaojihusisha na uzalishaji na usambazaji wa nishati safi.

"Huwezi kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa bila kuleta mabadiliko ya nishati ya kupikia. Ufadhili wa EU unalenga ubunifu wa teknolojia ya kisasa ya kupata majiko yanayotumia mkaa, gesi na kuni kidogo. "Tunatoa ruzuku kwa kampuni ili mtumiaji wa mwisho aweze kupata nishati na jiko kwa bei ndogo," alisema.

Muro alisema ufadhili huo unalenga kusaidia biashara ya nishati safi ya kupikia ambayo ni rafiki wa mazingira, ili kuchangia juhudi za kidunia za maendeleo endelevu na kuokoa mazingira.

Alisema kampeni ya 'Anzia Jikoni' inalenga kuueleza umma umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kupikia zinazopunguza madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Muro alitaja baadhi ya teknolojia ambazo zimeshavumbuliwa kwa ajili ya kupikia kuwa ni mkaa na kuni mbadala, majiko ya gesi yanayotumia kiasi kidogo cha nishati hiyo, mafuta (bioethanol) kwa ajili ya kupikia na jiko la umeme linalotumia umeme kidogo.

Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mradi wa Cookfund, Elizabeth Ngoye, alisema ndani ya miezi mitatu, watumiaji wapya 3,373 kutoka mikoa mitano inayohusika na mradi huo ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mwanza wamefikiwa na nishati safi ya kupikia.

# Sarakasi utatuzi mgogoro Kigamboni

**Na Faustine Feliciane**

SAKATA la mgogoro wa ardhi katika Kata ya Kimbiji, Manispaa ya Kigamboni limeibuka tena baada ya uamuzi wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla kubatilishwa na kutolewa uamuzi mpya na uongozi wa manispaa hiyo.

Mgogoro huo wa barabara inayotoka barabara kuu ya Kigamboni-Buyuni kwenda maeneo ya ufukwe wa bahari umekuwa wa muda mrefu baada ya mwekezaji kampuni ya ASM LTD kufunga barabara hiyo kwa kujenga ukuta na kuwafanya wananchi wa Kijiji cha Mikenge kushindwa kufika ufukweni kwa ajili ya shughuli zao za uvuvi.

Katika utatuzi wake, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Makalla, katika kikao cha pamoja kati ya wananchi na wawekezaji Desemba 16 mwaka jana, aliamuru barabara hiyo ifunguliwe kwa manufaa ya wananchi na mwekezaji huyo alipwe fidia kwa eneo litakalochukuliwa.

Katika barua yake ya Desemba 27, 2022 iliyoandikwa na Manispaa ya Kigamboni kwenda ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilielezea utekelezaji wa maagizo ya Mkuu wa Mkoa ya kufungua barabara hiyo.

Hata hivyo, akizungumza juzi katika mkutano wa wananchi wa eneo hilo, Mkuu mpya wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo, alisema uamuzi uliofikiwa baada ya vikao vya ndani ni kutafuta barabara mbadala ya kuwawezesha wananchi kufika katika ufukweni na wawekezaji wengine kufika kwenye maeneo yao.

"Ndugu zangu, ninaomba turidhie uamuzi huu, tumeamua kutafuta barabara mbadala ambayo itajengwa kutokana na makubaliano tuliyofikia na mwekezaji ASM anayelalamikiwa kuziba njia.

"Ninasema hivi kwa sababu hata mkikataa, huo ndio uamuzi wa mwisho na watendaji wetu wanaendelea na mchakato wa kujenga barabara hizo," alisema Halima.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, Erasto Kiwhale, alisema ujenzi wa barabara hizo utaanza ndani ya miezi mitatu na kuwataka wananchi kukubali uamuzi huo.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi walipinga uamuzi huo na kudai hakuna uwezekano wa kujengwa kwa barabara mpya kutokana na kuwapo korongo kubwa kuelekea baharini.

"Huu mgogoro tunaona unachangiwa na watendaji wetu wa manispaa. Mkuu wa Mkoa aliyepita (Makalla) alikuja hapa na akatembele maeneo yanayolalamikiwa pamoja na kukagua hizo njia wanazotaka kuzijenga sasa.

"Kwa kauli yake alisema ujenzi kwenye lile korongo hauwezekani na akatoa maagizo barabara iliyokuwa inatumika kwa miaka mingi ifunguliwe na huyu ASM alipwe fidia. Sasa huu uamuzi mapya umetokana na nini?" alihoji Mzee Mbwana Mwinyipingu, mkazi wa maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mikenge, Lameck Mayala, alisema wameshangazwa na uamuzi mpya wakati tayari mgogoro huo ulishatatuliwa. "Mimi sijui nini kinaendelea. Uamuzi ulishafikiwa na tulijua utekelezaji unaendelea. Leo wamekuja na uamuzi mpya, sijui nini hasa kinaendelea," alilalamika Mayala.

Mmoja wa wawekezaji wa hoteli ambaye ameathirika na kufungwa kwa barabara hiyo, Arif Sheikh, alisema eneo ambalo manispaa inataka kujenga barabara mpya, lina korongo lenye urefu unaofikia ghorofa tatu.

"Mheshimiwa Makalla alipaona na akakiri haiwezekani kujenga barabara hapo kwa sababu ujenzi wake ni gharama zaidi kuliko kulimpa fidia mwekezaji ASM ambaye hilo eneo hajaliendeleza,"alisema Arif.

Wananchi hao wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati mgogoro huo ili haki ipatikane.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu zianze maandalizi mapema msimu mpya

**MSIMU** wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/2023 umemalizika rasmi wiki iliyopita kwa Yanga kuchukua ubingwa kwa mara ya pili mfululizo.

Msimu huu uliomalizika tumeshuhudia ushindani mkubwa kwa klabu zote zilizoshiriki lakini pia tumeshuhudia mabadiliko makubwa kwenye ubora wa waamuzi wetu.

Msimu huu ndio msimu ambao malalamiko kwa waamuzi yamepungua ukilinganisha na misimu iliyopita ambapo waamuzi wetu walikuwa kwenye wakati mgumu kwa kulaumiwa kwa baadhi ya maamuzi yao uwanjani.

Kumalizika kwa msimu huu wa 2022/2023 ni maandalizi ya msimu mpya wa Ligi kuu na mashindano ya Kimataifa ambapo baadhi ya timu zetu zitaiwakilisha nchi.

Hiki ni kipindi kizuri kwa klabu zetu kufanya maandalizi mazuri ya ndani na nje ya uwanja ili kuleta ushindani mkubwa kwenye ligi na mashindano ya kimataifa kwa timu zitakazoshiriki.

Tayari tumejua timu zitakazoiwakilisha nchi kwenye mashindano ya Kimataifa, Yanga , Simba, Azam na Singida Fountain Gate FC zitashiriki kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Mashindano haya ni magumu na yanakutanisha timu kubwa Afrika zenye wachezaji mahiri na wenye uwezo mkubwa.

Klabu zetu lazima zijipange vizuri na kufanya maandalizi ya kutosha kuweza kukabiliana na timu nyingine za Afrika zitakazoshiriki mashindano hayo.

Tunatoa wito kwa klabu zetu kuanza maandalizi mapema, maandalizi hayo ni kuanzia kwenye usajili, kambi ya timu na mambo mengine yanayoendana na maandalizi.

Maandalizi haya sio tu kwa klabu zitakazoshiriki mashindano ya CAF, bali kwa timu zote zitakazoshiriki Ligi Kuu msimu wa 2023/2024.

Tunataka kuona ligi msimu ujao ikiwa na ushindani mkubwa zaidi ya huu tuliouona msimu huu.

Ushindani huo unatokana hasa na maandalizi ya kila timu kuanzia kwenye usajili wa wachezaji, makocha na maandalizi ya ujumla kwa maana ya kambi na mazoezi.

Mpira ni mchezo wa wazi, mchezo ambao kile ulichokipanda kwa muda wa miezi zaidi ya miwili kitaonekana uwanjani.

Hakuna timu inayoshuka daraja au kushinda ubingwa kwa bahati mbaya, kushinda ubingwa ni mipango inayofanywa kwa muda mrefu kuanzia maandalizi ya Ligi .

Na timu inayoshuka daraja pamoja na changamoto nyingine, lakini huwezi kuondoa maandalizi duni kuelekea kwenye ligi, timu zetu lazima zijipange na kufanya maandalizi mazuri.

Jambo jema ni kwamba karibu mechi zote za ligi kuu zinaonyeshwa kwenye runinga, ni wazi mashabiki na wanachama wa klabu wataona kile ambacho timu zao kilifanya kwenye maandalizi ya msimu mpya.

Zipo timu zenye uwezo wa kwenda kuweka kambi nje ya nchi, maeneo ambayo ni mazuri kwa maandalizi yao, lakini bado timu nyingine hazipaswi kujiona 'wanyonge' kwenye maandalizi yao.

Ligi itachezwa kwenye viwanja vya ndani ya nchi, mazingira ni yale yale, hivyo kikubwa hapa ni muda wa kutosha wa kufanya maandalizi pamoja na kusajili vizuri.


Timu zisajili wachezeji kulingana na mahitaji yake, zisirundike wachezaji ambao wanajua kabisa hawawezi kuwatumia, lakini pia kwa wachezaji waangalie sehemu sahihi ya kwenda kucheza.

Tunazikumbusha timu kutumia vizuri kipindi hiki cha maandalizi kuelekea msimu mpya wa ligi kuu Tanzania Bara.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Simba ilizidiwa na Yanga kwenye fiziki ya wachezaji

**TANGU** Alhamisi iliyopita, Simba imekuwa ikitangaza kuachana na watu wake waliokuwa kwenye benchi la ufundi.

Iliachana na kocha wa magolikipa, Chlouha Zakaria, Kelvin Mandla ambaye ni kocha wa viungo, mtaalam wa viungo, Fareed Cassim na Kocha wa timu ya wanawake, Simba Queens, Charles Lukula.

Mimi najikita zaidi kwenye timu ya wanaume tena kwenye eneo la stamina na pumzi. Moja kati ya sehemu ambazo Simba itakuwa imecheza heko ni kumtimua Mandla na mtaalam wa viungo, Fareed. Inawezekana ikawa Mandla hana tatizo sana, lakini ilimpasa na yeye atoke ili watu watakaokuja waanze upya, na pia waje watu ambao Kocha Mkuu, Roberto Oliveira anawafahamu na kuwaamini ili afanye nao kazi kwa uhakika na uaminifu zaidi.

Nikianza kwa Fareed naona huyu alifeli tangu mwanzo kwa sababu Simba ndiyo timu iliyokuwa inazalisha majeruhi wengi zaidi. Nadhani kila mechi mbili ilikuwa lazima ipate mchezaji majeruhi. Na cha kushangaza zaidi walikuwa wanachukua muda mrefu kupona.

Hii yote mjibuji alikuwa ni mtaalam wa viungo, inakuwaje timu inakuwa na wachezaji majeruhi kila kukicha ambao wanachukua muda mrefu kurejea uwanjani?.

Pamoja na sababu zingine, lakini inaonekana hawakuwa na utimamu wa mwili, hii inakwenda kwa kocha wa viungo, ni ukweli usiopingika kwa misimu miwili hivi Simba imekuwa na wachezaji goigoi, ambao hawana nguvu, pumzi wala stamina. Walikuwa wanabebwa zaidi na majina, ustaa uwezo wao binafsi wa kusakata kambumbu.

Ukiangalia timu zote zilizokuwa zinacheza Ligi Kuu, ni Simba pekee iliyokuwa na wachezaji mmoja mmoja wenye uwezo mkubwa, lakini tatizo lilikuwa kwenye utimamu wa mwili.

Alianza kocha wa viungo Sbai Karim raia wa Tunisia, ambaye hakufua dafu, akaja Msauzi Mandla ambaye naye akachemka.

Kwa hali ya kawaida isingewezekana kocha huyo kuwarudisha wachezaji wawe na utimamu wa mwili kwa asilimia 100 wakati timu ipo kwenye mashindano.

Mazoezi ya kuwajengea wachezaji pumzi na stamina huanza kwenye kipindi kinachoitwa 'pre season', ambapo wiki mbili au tatu za mwanzo, wachezaji wanafanyishwa mazoezi makali, magumu bila kugusa mpira ili kuwafanya wawe fiti, wawe tayari kwenye kupambana na kuwafanya wasiwe na majeraha ya mara kwa mara.

Kwa misimu miwili kwenye klabu ya Simba, kipindi hicho walikuwa wanawapeleka 'pre season' wachezaji ambao wanatarajiwa kuwatema, halafu wale wanaowasajili wanakuja kujiunga wakati kipindi hicho kimeisha. Hicho ni kichekesho.

Kwa kawaida kile ni kipindi ambacho tayari kocha anatakiwa kuwa na wachezaji wake wote ambao amewasajili kwa msimu mpya wa mashindano.

Haikuwa hivyo kwa upande wao. Wengine wakasajiliwa na kujiunga wakati 'pre season' imeshamalizika.

Halafu wale waliopata mazoezi hayo wakaachwa, Kichekesho kingine hicho.

Enzi za kina Luis Miquissone ambapo kocha wa viungo alikuwa Adel Zrane, wapinzani hata kama wanaongoza bao 1-0 dakika ya 70, Simba ilikuwa na uwezo wa kurudisha na kuongeza mengine hata matatu. Walikuwa wako fiziki na pumzi ya hali ya juu, Kilichowaumbua ni kuja kwa kocha Robertino ambapo aina yake ya soka ilihitaji wachezaji wawe na fiziki na pumzi ya kutosha.

Ndiyo maana wachezaji wengi walionekana kuchemka. Afadhali baadaye kidogo walianza kubadika, hicho ndicho kwa asilimia kubwa kilichowaangusha Simba msimu huu tofauti na wapinzani wao wa jadi Yanga.

Moja kati ya watu muhimu Yanga ni Mtunisia, Helmy Gueldich, ambaye aliwafanya wachezaji wa timu hiyo kuwa na fiziki kiasi cha kuweza kuzitetemesha hata timu za Afrika Kaskazini maarufu kama 'waarabu.'



Wafanyakazi wa Kampuni ya Sukari Kilombero wakishiriki katika uzinduzi wa msimu wa uzalishaji 2023/24 katika hafla iliyofanyika hivi karibuni. Tukio la uzinduzi wa uzalishaji baada ya msimu wa mvua ni hatua muhimu kuelekea msimu wa uzalishaji wa sukari ambao huchangia uzalishaji wa ajira za msimu, huku kampuni ikiwa na lengo la kuzalisha tani 129,080 za sukari kwa mwaka huu mpya. Mtu anayeweka miwa katika mashine ni Mkuu wa Uboreshaji Biashara, Hans Babylone huku akishuhudiwa na Mkuu wa Uzalishaji, Etienne Rousseau (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMONGSCO: Uamuzi huu serikali ingeua shule binafsi

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha Wamiliki na Mameneja wa Shule na Vyuo Binafsi nchini (TAMONGSCO) kimesifu uamuzi wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kukubali kukaa nao kufanya marekebisho ya tamko lake la kuzuia watoto wadogo kukaa bwenini.

Kimeutaja uamuzi huo uliotolewa kupitia waraka rasmi wa serikali uliotiwa saini na Kamishna wa Elimu, kwamba ungeua shule binafsi nyingi nchini.

Jijini Dar es Salaam juzi, Mwenyekiti wa Taifa chama hicho, Alfred Luvanda, alisema katika mkutano uliohusisha viongozi mbalimbali wa shule binafsi na serikali, kuwa wameamua kuwasilisha vikwazo vyao ili vitafutiwe ufumbuzi.

Alisema tamko la waziri lililowataka kufunga shule za bweni kuanzia darasa la kwanza hadi la nne liliibua sintofahamu kubwa kwa wazazi na wamiliki wa shule binafsi hasa zenye huduma ya malazi.

"Ninaweza kutoa mfano kidogo, unakuta askari ana mtoto anasoma na kituo chake cha kazi labda ni Sudani, yuko Darfur. Hakuna namna yule mtoto atapata malezi mazuri zaidi ya shuleni, kwa sababu nyumbani uangalizi wake unakuwa mdogo.

"Dada mdogo amepata ujauzito, anafanya kazi Kariakoo na makazi yake yapo Mbagala na mtoto unakuta pengine amesuswa amtunze peke yake. Eneo sahihi kwa yule mtoto kupata malezi ni shuleni," alifafanua.

Mwenyekiti huyo alisema kwa sasa wamepewa mwongozo na serikali ambao kwa mtazamo wake "upo vizuri". Aliutaja unaruhusu watoto wanaotoka mazingira hatarishi wabaki shule za bweni. Serikali imetambua vipo vikwazo kwa watoto wote kuzuiliwa kusoma katika shule zenye huduma ya malazi.

Mgeni rasmi katika mkutano huo, Prof. Anna Tibaijuka ambaye ni mbunge aliyewahi kuwa waziri, alisema sasa ni wakati wa kutambua mchango mkubwa unaofanywa na shule binafsi katika kuinua elimu nchini.

Pia alishauri shule binafsi ziwekeze zaidi katika utoaji wa elimu ya sayansi kwa vitendo ili kuandaa kizazi kinachokwenda na wakati huu wa zama za kidigitali.

"Serikali tunaangalia namna ya kuziwezesha shule binafsi kupata mikopo nafuu, ili shule hizi ziwekeze katika maabara na elimu ya vitendo, na ushauri wote utakaotolewa katika mkutano huu nitaufikisha kwa wahusika wakuu ili ufanyiwe kazi," aliahidi.

Vilevile, alisifu kitendo cha benki mbalimbali zikiwamo CRDB, NMB, NBC, Benki ya Maendele na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa kuunga mkono juhudi za shule binafsi katika kutekeleza adhima yao ya kutoa elimu bora. Wadau wengine waige mfano huo.

Mwanzoni mwa Machi mwaka huu, Wizara ya Elimu ilitoa waraka wa kuzitaka shule zote zinazotoa huduma ya bweni kwa madarasa ya awali hadi la nne kusitisha huduma hiyo ifikapo mwisho wa muhula wa kwanza mwaka 2023.

Waraka huo uliotolewa na Kamishna wa Elimu wa wizara hiyo, Dk. Lyabwene Mtahabwa kwa wadau wa elimu nchini, unaelekeza hairuhusiwi kutoa huduma ya bweni kwa wanafunzi wa elimu ya awali hadi darasa la nne isipokuwa kwa kibali maalum kitakachotolewa na Kamishna wa Elimu baada ya kupokea maombi kutoka mdau husika.

## NBC yazindua akaunti maalum kwa walimu

**Na Joseph Mwendapole**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imezindua akaunti mpya inayojulikana kama 'Akaunti ya Mwalimu', ikilenga kutoa suluhisho la huduma za kifedha zenye gharama nafuu kwa walimu nchini.

Akaunti hiyo ya kibunifu inalenga kutoa faida na huduma maalum zilizobuniwa kwa ajili ya mahitaji ya kipekee ya walimu na kuwawezesha kufanikiwa kutatua changamoto mbalimbali za kifedha.

Wakati ya hafla ya uzinduzi huo, Mkuu wa Fedha na Masoko ya Kigeni wa benki hiyo, Juliana Mwapachu, alisema Akunti ya Mwalimu inawakilisha hatua muhimu katika safari ya kujumuisha kifedha na kuwawezesha walimu.

Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa na Wateja Binafsi, Abel Kaseko, alisema Akaunti ya Mwalimu ni suluhisho la benki la kipekee lililobuniwa kwa ajili ya walimu nchini.

"Hii inatoa huduma kamili ya bidhaa na huduma za kifedha zilizobuniwa kwa mahitaji ya jamii ya walimu, ikitoa udhibiti mkubwa wa fedha zao na fursa ya kujenga mustakabali imara," alisema.

Aliongeza kuwa kupitia ushirikiano wa NBC na Samsung, walimu watapata punguzo la hadi asilimia 10 katika ununuzi wa kifaa chochote kutoka maduka ya Samsung na pia kuna punguzo lingine la hadi asilimia 15 katika ununuzi wa paneli za nishati ya jua na pikipiki.

"Akaunti ya Mwalimu inalenga kubadilisha uzoefu wa benki kwa walimu kwa kutoa faida nyingi ikiwamo kutotozwa ada ya kila mwezi, tunaelewa umuhimu wa urahisi na matumizi rahisi kwa walimu, hivyo tumefuta ada yoyote ya matunzo yanayohusiana na akaunti hii.


"Pia tumeondoa ada ya shughuli iliyowekwa bila kujali kiasi cha shughuli au njia iliyotumika, walimu watapata ada iliyowekwa ya Sh. 2,000 tu kwa aina zote za shughuli, kutoa uwazi na gharama nafuu," alisema. Alitaja faida ya akaunti hiyo kuwa ni pamoja na familia kupokea faida ya elimu ya Sh. milioni sita mwalimu anapofariki dunia kuhakikisha mahitaji ya elimu ya watoto yanatimizwa wakati wa kipindi kigumu kama hicho.

Alisema benki pia itatoa mkono wa pole kama ishara ya msaada katika tukio la kufariki dunia kwa mwalimu kwa kutoa malipo ya rambirambi ya Sh. milioni mbili.

Alisema katika tukio baya la mwalimu kupata ulemavu wa kudumu, benki itatoa Sh. milioni mbili kama ishara ya msaada na kwamba Akaunti ya Mwalimu inakuja na programu ya benki ya simu inayoweza kutumika kwa urahisi.

Vilevile, alisema akaunti hiyo itaruhusu walimu kupata akaunti zao, kufanya shughuli na kusimamia fedha zao kwa urahisi kupitia simu zao za mkononi.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Ilivyo Tuzo ya Miundombinu Afrika, namna ADB ilivyomtunuku Dk. Samia

## -Mwanamke wa kwanza, wa tatu Afrika Mashariki

Na Mwandihi Wetu

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan mwaka jana amepokea tuzo iitwayo Babacar Ndiaye, akikabidhiwa kwa mwaka 2022 kutoka kwa Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Solomon Quaynor, kwa niaba ya Rais wa Benki hiyo, Dk. Akinumwi Adesina.

Amepewa Tuzo ya Babacar Ndiaye kwa mwaka 2022 (Babacar Ndiaye Trophy 2022), kutambua jitihada anazozifanya kujenga miundombinu nchini, akiwa katika orodha ya viongozi 100 wenye ushawishi mkubwa duniani, kwa mujibu wa jarida moja.

Kamati ya uteuzi wa tuzo hiyo imempongeza Rais Samia kwa uongozi na namna serikali yake ilivyojipanga kuwezesha sekta ya miundombinu nchini Tanzania."Ni kwa uongozi wake binafsi, uwekezaji mkubwa na kujitolea katika kupanua barabara na mtandao wa reli nchini Tanzania. Tunatuma pongezi zetu za dhati kwa Rais Samia Suluhu Hassan na watu wa Tanzania," anatamka msemaji wa Taasisi ya ARB, George Orido.

Orido anasema kamati ilibaini fedha dola milioni 290 zilizotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, kusaidia kufufua usafiri wa barabara, reli na anga nchini Tanzania na zimeleta matokeo bora.

Pia anataja kuzingatiwa mkataba wa dola milioni 172.2 uliotiwa saini na kampuni ya kichina, kuipatia nchi mabehewa ya kisasa ya mizigo 1,430 ili kutekeleza mpango Shirika la Reli la Tanzania (TRC).

Inatamkwa, kamati ilibaini kuanza rasmi ujenzi wa mradi wa kihistoria wa barabara ya mzunguko wa nje mjini Dodoma, uliozinduliwa na Rais Dk. Samia, Februari mwaka jana na kuhudhuriwa na Rais wa sasa wa Benki ya Maendeleo Afrika, Dk. Akinwumi Adesina.

Tuzo hiyo hutolewa kwa watu mashuhuri duniani wanaoonyesha dhamira kuendeleza sekta ya miundombinu ya usafiri.

Mkuu huyo wa nchi amekabidhiwa tuzo hiyo Mei, 2022 katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 57 wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), nchini Ghana kujadili fursa na changamoto zaAfrika.

Kimsingi, ni sehemu ya uendelezaji kimradi, katika ebneo la miundombinu, ambayo katika mfumuko wa kiutawala na kisera, ikioanishwa na mwongozo kutoka chama tawala, CCM kila awamu ya uongozi inapokezana kijiti kuendeleza yale ya kisera na ilani iliyopo.

Vilevile, inatajwa kiongozi wa awamu husika anayekuwapo madarakani, anakuwa na yake kimaono na ubunifu kama hayo yanayotajwa kutoka kwa Rais Dk. Samia, hata kumfikishia ujumbe kimataifa unaomkaribishia tuzo ya mwaka jana.

### ANENACHO DK. SAMIA

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Dk. Samia anasema tuzo hiyo ina hisia mchanganyiko, kwa sababu anao uhakika kuwa kwa muda ambao amekaa madarakani usingeweza kumfanya yeye kupata tuzo hiyo.

Hiyo ni kutokana na kile alichoeleza kuwa ujenzi wa miundombinu huhitaji muda zaidi, kwani kuanzia upembuzi yakinifu unapofanyika, hadi fedha zinapopatikana, si rahisi kusema ndani ya zaidi ya mwaka mmoja aliokaa angefanikisha hayo.

"Miradi inachukua miaka mingi, ni mchakato endelevu, kwetu sisi ulianzia awamu ya kwanza hadi ya tano, mengi yalifanyika ikiwamo kupanua mtandao wa barabara na kuunganisha maeneo mbalimbali ya nchi katika kipindi cha awamu ya nne kilichoongozwa na Jakaya Kikwete,"anafafanua.

"Katika jitihada hizi, mtu mmoja alijitokeza ziadi nyakati hizi zote na huyu ni John Pombe Magufuli (Rais wa awamu ya tano) mtangulizi wangu, alitumika katika awamu ya tatu na nne kama Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, kabla ya kuwa kiongozi mkuu wa Taifa ili aendeleza jitihada hizo.

"Ni bahati mbaya hayupo nasi aweze kushuhudia matunda ya jitihada na uongozi wake. Tuzo hii inatupa msukumo viongozi wa Afrika kufanya kazi kuendeleza barabara na reli kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi wetu," anafafanua.

Baadhi ya waliowahi kupata tuzo hizo inayojumuisha wakuu wa nchi za Rais wa Morocco, Zambia, Ivory Coast, Ethiopia na Gabon katika mwaka huo wa kwanza 2016.

Baadaye wakafuata marais; mwaka 2017, Macky Sall wa Senegal na Paul Kagame wa Rwanda; 2018, ikawa zamu ya Uhuru Kenyatta na Adama Barrow wa Gambia mwaka 2019; huku mwaka juzi ikamwangukia Rais Abdel Fattah Al-Sisi wa Misri.

Mwaka juzi ulikuwa kwa Rais Muhammadu Buhari wa Nigeria, kabla ya kumfikia Dk. Samia, mwaka jana, akiwa na upekee wake, rais wa kwanza mwanamke kupokea tuzo hiyo.

Akikabidhi tuzo hiyo kwa Dk. Samia, Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda katika Benki ya Maendeleo ya Afrika, Solomon Quaynor anasema ni vyema viongozi wa Afrika kufikiria kuhusu barabara za kikanda za ndani, kwani haiwezekani kuiunganisha Afrika kiuchumi.

"Tunataka ukanda huru wa biashara wa Afrika uweze kufanya kazi, tumetaja sekta ambazo nazishughulikia, sekta ya viwanda na miundombinu zote tunazishughulikia, siyo tu kufanya biashara kwa ajili ya kusafirisha mizigo, pia kuongeza thamani kwa kusaidia viwanda vidogo hasa katika mnyororo wa thamani katika kilimo," anatamka.




Siku Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipopokea Tuzo ya Miundombinu ya Babacar Ndiaye, mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

### MZIZI WA TUZO

Tuzo ya Babacar Ndiaye, inatokana na aliyekuwa Mkuu wa Benki ya Afrika, Babacar N'diaye, ikitungwa kwa jina lake, inayoangaza maendeleo ya ujenzi wa barabara, kwa ushirika na Umoja wa Wanahabari za Miundombinu na Fedha barani Afrika(MIFA).

Mzaliwa huyo wa mwaka 1938 na akafariki mwaka 2017, ni msomi aliyeanza kutumikia chombo hicho mwaka 1086, akapanda cheo hadi kuwa Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Afrika, baadaye Makamu wa Rais wa chombo hicho, mwaka 1985, hata akakwea zaidi kuwa Rais, kipindi chake kukihesabiwa mafanikio makubwa hadi kufika mwaka 1987.

Maboresho yanayotajwa chini yake ni mageuzi makubwa ya ufanisi wa chombo hicho, ikiwamo kutanuka mtaji kwa asilimia 200, kufikia dola za Marekani bilioni 23.3, huku kukianzishwa kitengo maalum cha maendeleo ya sekta binafsi.

Pia Quaynor anatajwa kubuni chombo cha benki hiyo kinachohusika na Huduma ya Ndani na Nje kibenki, hali kadhalika Meza Maalum ya Kibenki, inayojadili mustakabali wa biashara Afrika.

Babacar Ndiaye alihitimisha utumishi wake katika Benki ya Afrika mwaka 1995 na akafariki mwaka 2017, akiwa nyumbani kwao nchini Senegal, akiwa na usemi wa kiitikadi aliyoubuni na kupenda kutamka 'Senegal ni kijijini kwetu na Afrika ni nchi yangu."

"Ni bahati mbaya hayupo nasi aweze kushuhudia matunda ya jitihada na uongozi wake. Tuzo hii inatupa msukumo viongozi wa Afrika kufanya kazi kuendeleza barabara na reli kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi wetu," anasema Dk. Samia.

Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda katika Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Solomon Quaynor, anasema ni vyema viongozi wa Afrika kuanza kufikiria kuhusu barabara za kikanda na za ndani.

"Tunataka ukanda huru wa biashara wa Afrika uweze kufanya kazi, tumetaja sekta ambazo nazishughulikia, sekta ya viwanda na miundombinu zote tunazishughulikia," anatamka na kuhitimisha kuwa: "Siyo tu kufanya biashara kwa ajili ya kusafirisha mizigo, pia kuongeza thamani kwa kusaidia viwanda vidogo hasa katika mnyororo wa thamani katika kilimo."



## HABARI DODOMA

## Vyama ushirika vyaonywa ubadhirifu fedha za miradi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imevitaka vyama vya ushirika nchini kuinua uchumi wa wananchi badala ya kuwa sehemu ya ubadhirifu wa fedha za miradi wanazokabidhiwa na wafadhili kwa ajili ya maendeleo.

Imesema hali hiyo imesababisha baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kuishia mikononi mwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) pamoja na Jeshi la Polisi.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, wakati akizindua mradi wa Haki ya Chakula na Ubora wa Maisha wenye thamani ya Sh. bilioni 9.3 unaotekelezwa kwa miaka mitano na shirika lisilo la kiserikali la We Effect katika mikoa sita nchini.

Mavunde alisema vyama vingi vya ushirika vimekuwa na migogoro mingi sana na washirika wake hususani wakulima na wafugaji jambo ambalo linachangia kutokea ubadhilifu wa fedha ikiwamo kuleta migogoro na kurudisha nyuma maendeleo ya walengwa hao ambayo yamekusudiwa na wafadhili wanaotoa fedha.

Hivyo, aliwataka kuondoa makandokando na kutumia fedha hizo vizuri ambazo zimetolewa na serikali ya Sweden kupitia shirika lake la maendeleo (SIDA) kwa ajili ya kutekeleza mradi huo katika mikoa husika ambayo imetajwa ili kuhakikisha mradi huo unapokamilika ulete matokeo chanya kwa wananchi wa maeneo husika.

Alisema mradi huo ambao unakwenda kutekelezwa umehusisha watu wa sekta ya kilimo, ufugaji ambao wote wanafanya kazi pamoja na vyama vya ushirika, hivyo ametoa rai wakafanye kazi kwa ushirikiano ili kuhakikisha wanaweka mipango bora ya matumizi ya fedha hizo.

Pia aliwataka viongozi wa vyama ambao wamesaini kwa ajili ya kupatiwa fedha za utekelezaji wa mradi huo kwenda kuzitumia katika matumizi sahihi ili ziweze kuleta matokeo chanya ambayo yatawashawishi wafadhili hao kuendelea kutoa fedha nyingine kwa ajili ya kutekeleza miradi mingine kwa wananchi.

Mkurugenzi wa We Effect wa Kanda ya Afrika Mashariki, George Onyango aliishukuru serikali kutokana na ushirikiano inaoonyesha katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za shirika hilo hapa nchini.

Onyango alisema fedha hizo zitumike ipasavyo kwa lengo lililokusudiwa kwa sababu shirika lao liko wazi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali wanayofanya kwa kushirikiana na wafadhili pamoja na serikali.

Alisema SIDA wametoa fedha hizo wanahitaji kuona zinafanya maendeleo yaliyokusudiwa kwa walengwa.

# Ummy aagiza vituo vya afya kuwa na majokofu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu ameviagiza vituo vya afya vinavyotoa huduma za upasuaji kwa wajawazito kuwa na majokofu ya kuhifadhia mazao ya damu (plasma) ili kusaidia kupunguza vifo vya wajawazito wakati wa kujifungua.

Alitoa agizo hilo juzi jijini hapa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uchangiaji Damu Duniani pamoja na uzinduzi wa Kituo cha Damu Salama Kanda ya Kati.

Alisema ili kuondokana na vifo vya wajawazito wakati wa kujifungua vituo vyote vya afya nchini vinapaswa kuwa na majokofu ya kuhifadhia mazao ya damu.

"Kinamama wengi wamekuwa wakipoteza maisha yao wakati wa kujifungua kutokana na kutokwa damu nyingi pamoja na uwepo wa sindano zinatumika kuzuia kutoka kwa damu lakini uwepo wa damu katika kituo ni jambo la lazima sana ili kuokoa maisha ya mama," alisema Ummy.

Alisema sababu nyingine ya vituo hivyo kuwa na majokofu ya kuhifadhia mazao ya damu ni kutokana na damu kuwa na uwezo wa kutumia ndani ya siku 45 pekee na baada ya muda huo inaharibika.

"Damu baada ya mtu kuchangia na kuhifadhiwa kwenye kituo cha damu salama inaweza kutumika ndani ya siku 45 na baada ya hapo inaharibika hivyo kutokana na teknolojia kukua inaweza kutengenezwa mazao ya damu (plasma) na kuwa na uwezo wa kudumu kwa mwaka mmoja," alisema.

Aidha, aliagiza halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya kuhamasisha na kukusanya damu katika maeneo yao ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

Alisema jukumu la kukusanya damu ni la kila halmashauri hivyo wahakikishe wanatenga bajeti ambayo itawawezesha kukusanya damu na kuihifadhi katika benki zao kwa ajili ya matumizi.

"Leo hii halmashauri ukisikia kuna mechi ya Simba na Yanga peleka timu watu wachangie damu, ukisikia kuna tukio la serikali peleka timu pia watu wachangie na hili liwe ni kipaumbele katika majukumu yenu ya kila siku kwani damu ni jambo la muhimu sana hakuna duka wala kiwanda kinachouza damu ni sisi wenyewe ndiyo tutachangiana," alisema.

Kadhalika, aliwataka Watanzania kuendelea kujitokeza kuchangia damu ili kufikia mahitaji ya chupa 590,000 zinazohitajika kila mwaka nchini.

Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Neema Kileo alisema maadhimisho ya siku hiyo yanalengo la kuwakumbuka watu ambao wamekuwa wakichangia damu na kuokoa maisha.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa nchi nyingi katika Bara la Afrika hivi sasa zimepiga hatua kwenye ukusanyaji, uhifadhi na usambazaji wa damu.

"Utafiti pia unaonyesha katika Bara la Afrika ni nchi nane pekee ndiyo zenye vitengo bora vya utoaji huduma za damu salama na Tanzania ikiwa ni mojawapo ya mataifa hayo," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Grace Maghembe, alisema kutokana na kuongezeka kwa vituo vya utoaji wa huduma za upasuaji wajawazito nchini mahitaji ya damu yanazidi kuongezeka.

Alisema kituo cha damu salama kilichozinduliwa Kanda ya Kati kitasaidia kuboresha huduma za afya katika mikoa ya Singida, Dodoma na maeneo jirani kutokana na huduma za mbalimbali kutolewa ikiwamo upimaji wa sampuli za damu.



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo akisaidia kuweka udongo kwenye mashine ya kufyatulia tofali kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya Kata ya Kingiti Wilaya ya Mpwapwa Mkoani Dodoma alipofika akiwa kwenye ziara ya kutembelea jimbo la Kibakwe jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yatoa Bil. 34/- ujenzi wa miundombinu ya skimu

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

SERIKALI kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetoa Sh. bilioni 34.176 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya skimu ya msingi iliyopo Kata ya Msingi wilayani Mkalama mkoani Singida.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, katika hafla ya makabidhiano ya eneo la mradi wa skimu hiyo juzi ujenzi wake unaanza mwezi huu, alisema juzi kuwa mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wananchi 12,000 kutoka vijiji vinne vya Ishinsi, Ndurumo, Msingi na Kidi.

Alisema Mkoa wa Singida una eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta 44,619 lakini eneo lililoendelezwa kwa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji ni hekta 3,053 tu sawa na asilimia 6.84 na wakulima wanaonufaika na kilimo cha umwagiliaji ni 6,500 tu.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2023/24 umepanga kutekeleza miradi mingi ya kilimo cha umwagiliaji itakayokuwa na uwezo wa kumwagilia hekta 32,018 sawa na asilimia 65.85 ya eneo la hekta 44,619 linalofaa kwa kilimo hicho mkoani humo.

Serukamba alisema hekta 32,018 zitakapolimwa katika msimu huo zitawanufaisha wakulima 80,045 watakaolima kwa zaidi ya msimu mmoja katika kipindi cha mwaka na hivyo kuinua kipato chao, mkoa na taifa kwa ujumla.

Mkuu huyo wa mkoa aliwaeleza wananchi wa vijiji hivyo kuwa wasiuze ardhi kwa watu wengine hali itakayosababisha wanufaike watu kutoka nje ya kata na wilaya hiyo wakati lengo la serikali ni kutaka kuona wananchi wa Kata ya Msingi ndio wanakuwa wanufaika wa mradi huo. Aidha, aliwaondoa hofu kuwa hakuna mwananchi atakayenyang'anywa ardhi na kuwaagiza wenyeviti wa vijiji hivyo kuhakikisha wanaorodhesha majina ya wananchi wao ili kila mmoja apate eneo la kulima.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Raymond Mndolwa, alisema hivi sasa serikali imeongeza bajeti katika sekta ya kilimo cha umwagiliaji kutoka Sh.bilioni 46 zilizotolewa 2018/2019 hadi kufikia Sh.bilioni 365 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 693.

Alisema pamoja na kwamba siyo jukumu la tume hiyo kujenga barabara lakini katika mradi huo zimetengwa fedha kwa ajili ya kujenga kilometa nane ili kuwawezesha wananchi kupata urahisi wa kusafirisha mazao yao kutoka mashambani.

Alisema katika mwaka wa fedha ujao tume hiyo itajenga ghala la kuhifadhia mazao katika kata hiyo ya msingi ili wakulima wakishavuna wanayahifadhi kwa ajili ya kusubiri kuyauza na kwamba ni jukumu la viongozi wa kijiji kutenga eneo litakapojengwa ghala hilo.

Mndolwa alisema wakati serikali inajenga miundombinu hiyo ya umwagiliaji wakulima wana wajibu wa kulipa ada ya umwagiliaji fedha ambazo zitakuwa zinawekwa kwenye akaunti maalum ambazo zitatumika kwa ajili ya ukarabati na uendelezaji wa sehemu nyingine zenye miradi hapa nchini.



## Mapato 'kiduchu' ya utalii yaishtua serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imewasilisha katika Baraza la Wawakilishi mapendekezo ya bajeti yake kwa mwaka 2023/24, ikijikita kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Akiwasilisha bajeti hiyo katika kikao cha baraza hilo juzi, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Salum Mkuya, alisema Zanzibar ina nafasi kubwa katika kukuza uchumi wa ukanda wa Afrika Mashariki.

Alisema bajeti hiyo imelenga kuinua uchumi wa wananchi visiwani humo na kuimarisha miundombinu ili kuvutia uwekezaji.

Waziri huyo alitaja maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kugharamia miradi ya kielelezo inayoendelea na ulipaji wa pensheni kwa wastaafu kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema maelekezo hayo aliyatoa Siku ya Wafanyakazi Duniani alipotangaza kuwaongeza pensheni wastaafu wa SMZ pamoja na Pencheni Jamii kwa asilimia 150.

Vilevile, alisema serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya barabara, kuimarisha huduma za jamii, uchumi wa buluu, bandari na viwanja vya ndege, mifumo ya usimamizi wa mapato yanayotokana na utalii na kulipa amana za wananchi waliyokuwa na amana katika Benki ya FBME.

Alisema Zanzibar ina fursa ya kipekee katika anga za kitalii kutokana na jina, mandhari, umahiri, mazingira na utamaduni wa watu wake.

"Maendeleo ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea kutokea, yanalenga pamoja na mambo mengine, kuhakikisha upekee wa Zanzibar katika taswira ya kitalii unaleta tija ya kiuchumi pamoja na maendeleo ya watu wake," alisema.

Waziri huyo alisema changamoto kubwa iliyopo kwa sasa ni ongezeko la watalii Zanzibar ambalo haliakisi mapato yanayoingia serikalini.

Alitoa mfano kuwa kati ya mwezi Julai 2021 na Juni 2022, mapato yaliyorekodiwa katika mifumo ya serikali yalifikia Sh. bilioni 69.89 na Julai 2022 hadi Machi 2023 yalikuwa Sh. bilioni 51.32.

Alisema serikali itaendelea na jitihada za kuweka sera sahihi na mikakati ikiwamo mifumo ambayo itahakikisha kuwapo uwiano madhubuti baina ya ongezeko la watalii na mapato yanayotokana na shughuli za utalii.

Alisema mapato ya serikali kwa mwaka fedha 2023/24 yanakadiriwa kufikia Sh. bilioni 2,840.85. Kati yake, Sh. bilioni 2,822.85 ni kwa Serikali Kuu na Sh. bilioni 18 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

"Makadirio haya yameongezeka kwa asilimia tisa kulinganishwa na makadirio ya mwaka 2022/23 ya Sh. bilioni 2,606.58," alisema.

Alisema serikali imekadiria kukusanya Sh. bilioni 1,419.03 kutoka katika vyanzo vya ndani ikiwa na ongezeko la asilimia nne kulinganishwa na makadirio ya kukusanya Sh. bilioni 1,369.75 makadirio ya mwaka 2023/2024.

"Mikopo ya ndani na nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ni Sh. bilioni 717.21. Ninaliomba baraza lako tukufu kuridhia Sh. bilioni 18 kukusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa," alisema.

# 'Teknolojia ya habari imebadili mwelekeo wetu wa kibiashara'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Ikulu, Jamal Kassim, amesema maendeleo makubwa ya teknolojia ya habari duniani yamesababisha kubadilika kwa mwelekeo wa kibiashara.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akifungua warsha ya uzinduzi wa mwelekeo wa Mpango wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidigitali kwa Zanzibar (Zanzibar Digital Economy Roadmap).

Alisema kutokana na mabadiliko hayo ni vyema nchi zibadilike ili ziendane sambamba na mabadiliko ya biashara kuwa ya kidijitali.

Kassim alisema kihistoria asili ya Zanzibar ni nchi ya uchumi wa kibiashara na wafanyabiashara kutoka mashariki ya mbali ambao walikuwa wakileta bidhaa zao na zile za visiwani humo kusafirishwa.

"Zanzibar isingepata sifa ya upekee bila ya mchango wa biashara hii ya kimataifa, na uchumi wa Zanzibar tangu asili umetokana na biashara," alisema.

Aliongeza kuwa mabadiliko hayo hayakubadilisha mwelekeo wa biashara tu pekee, bali pia kila eneo la maisha ya mwanadamu ambapo uchumi wote wa dunia umelazimika kuendeshwa kwa namna tofauti na ilivyokuwa zamani.

Waziri huyo alisema Zanzibar imejikita kwenye uchumi wa buluu, hivyo mabadiliko ya kidigitali ili kunufaika na uchumi huo.

Alisema wazo la kuwa na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar linaainisha namna serikali ilivyoona mbali katika kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia yaliyoifanya dunia kuwa ni kijiji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao, Seif Said Seif, alisema uchumi wa kidigitali ambao mwelekeo wake unazinduliwa ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuendesha shughuli zote za kiuchumi kwa kuunganisha kiufanisi na uchumi mwingine wa dunia.

Mkurugenzi Seif alisema wakala wa serikali mtandao kupitia mwelekeo huo utasaidia katika kuizindua jamii ya Wazanzibar namna ya kupanua wigo huo wa matumizi ya uchumi wa kidigitali.

Naibu Ofisa Mtendaji Mkuu kutoka Ofisi Ufatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini (PDB), Dk. Josephine Kimaro, alisema serikali kupitia taasisi zake ina kila sababu ya kufurahia hatua hiyo ya kuwapo uchumi wa kidigitali Zanzibar.

Alisema uchumi wa kidigitali utasaidia kuongeza mapato ya serikali kutokana na kuongezeka kwa ufanisi katika hatua zote muhimu za uendeshaji uchumi wenyewe.



Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Hemed Suleiman Abdulla, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, alipowasili katika ukumbi wa VIP Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar, akielekea Nchini Ujerumani kumuwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Uzinduzi wa Mashindano ya Dunia ya Olimpiki Maalum yanayofanyika Berlin Ujerumani. **PICHA: IKULU**

# ZEC kukabidhiwa jengo jipya

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeahidi kuipatia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) jengo jipya la kisasa litakaloendana na hadhi ya tume na kupatiwa ofisi za ngazi zote za wilaya.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alitoa ahadi hizo alipozungumza na viongozi wa tume hiyo Ikulu Zanzibar.

Aliipongeza tume hiyo kwa ushirikiano walioutoa kwa wadau wakiwamo vyama vya siasa pamoja na kufanikiwa kutangaza matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2020 ndani ya saa 24 baada ya uchaguzi kumalizika.

Alisema serikali inajipanga na kuifanyia kazi changamoto ya vyombo vya usafiri inayoikabili tume na kuahidi kuongeza bajeti itakayofanikisha utendaji wake.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mkuu mstaafu Hamid Mahmoud, alisema tume ilipewa majukumu ya utendaji kazi chini ya sheria tatu ambazo ni Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Mwaka 2019, Sheria ya Uchaguzi Na. 4 ya Mwaka 2018 na Sheria ya Kura ya Maoni Na. 6 ya Mwaka 2000.

Alisema sheria inaitaka tume kumkabidhi ripoti ya utendaji kwa Rais wa Zanzibar baada ya kukamilisha muda wake wa utumishi.


Mbali na mafanikio makubwa yaliyofikiwa, tume hiyo ilimweleza Rais Mwinyi kwamba ilifanikiwa kuandaa muundo mpya wa ofisi ya tume uliotoka kwa utumishi wa tume ukiwamo muundo wa mishahara uliozingatia maslahi ya watumishi wa tume.

Tume hiyo ilisema ndani ya miaka mitano ya utumishi wake ilifanikiwa kufanya kazi kwa ushirikiano na ufanisi mkubwa na vyama vya siasa nchini pamoja na kufanikiwa kuandaa mpango mkakati wa miaka mitano kuanzia mwaka 2022 hadi 2026.

Pia ilifanikiwa kuandaa na kusimamia uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kupitia fedha za mfuko mkuu wa serikali na ilifanikiwa kutekeleza haki na misingi ya demokrasia kwa kushirikisha matumizi ya TEHAMA na ushirikishwaji wa wadau katika masuala yote ya uchaguzi.

Licha ya mafanikio hayo, tume ilimweleza Rais Mwinyi changamoto iliyokumbana nazo kubwa ikiwa ni kutokuwa na ofisi za uhakika Unguja na Pemba hata kwa ngazi za wilaya.

Alisema hali hiyo ilisababisha kuathiri utendaji. Pia kuna changamoto ya vyombo vya usafiri na maslahi ya watendaji wake pamoja na ukosefu wa bajeti, hasa kwa asasi za kiraia.



**DIAMOND**

UKURASA 12



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# HITIMISHO DNA PEKEE

SAKATA la mfalme wa taarabu nchini, Mzee Yusufu na kijana anayeitwa Hamad ambaye anadai ni mtoto wake, linazidi kupamba moto baada ya mtoto huyo kudai anataka kufanyike uchunguzi wa vinasaba (DNA) ili kujiridhisha mashaka yake.

Katika mahojiano na radio ya Wasafi ya jijini Dar es Salaam, Hamad (21) anadai yeye ni mtoto wa Mzee Yusuph kulingana na maelezo ya mama yake ambaye kwa sasa ni marehemu.

Hata hivyo Mzee Yusuph, amejibu tuhuma hizo akisema yuko tayari kufanyiwa kipimo hicho, kwa sharti moja la mchakato huo uendeshwe kisheria na sio kutumia chombo cha habari kama inavyofanyika sasa.

Hamad amedai kwamba kwa muda mrefu amekuwa akipigana kutambuliwa na baba yake huyo, lakini hatua hiyo imekuwa ngumu kutokana na Mzee Yusuph kutokuwa tayari kumtambua.

“Ninachohitaji baba yangu (mzee Yusuph) kunitambua tu kuwa mimi n mwanawe, sina haja na mali wala jambo lolote, kwangu mimi kumjua baba ni suala la faraja.” Amesema Hamad.

Amesema anachohitaji kwa sasa ni kufanyiwa uchunguzi wa DNA kujua kama kile alichoambiwa na mama yake kuwa ni kweli au hapana, ili suala hilo lifike tamati na kila mtu aendelee na maisha yake.

Kwa upande wa Mzee Yusuph, amesema kijana huyo amemfahamu kwa muda mrefu na amekuwa akimsaidia kama watoto wengine, lakini anaamini sio mtoto wake kama anavyodai.

“Nilipokutana kwa mara ya kwanza na kuniambia mimi baba yake, nilimwambia anipe picha ya mama yake ili niweze kukumbuka, lakini hakufanya hivyo na badala yake anaendelea na madai yake hayo. Mimi nimekubali nipimwe DNA, lakini kwa sharti la mchakato wote uwe wa kisheria na kama itaonekana si mtoto wangu anilipe fidia ya kunidhalilisha,” amesema Mzee Yusuph.

BASI SAWA

## Diamond, Nameless kutumbuiza Uganda



WASANII nyota Afrika Mashariki, Diamond Platnumz na Nameless, wanatarajiwa kufanya kazi katika tamasha litakalofanyika mwezi Julai nchini Uganda.

Tamasha hio litakalofanyika tarehe 14, katika ukumbi maarufu wa Kololo litakuwa la kwanza kwa wababe hao wawili kukutana kwenye ukumbi mmoja.

Diamond kutoka Tanzania na Nameless kutoka Kenya ndio watakuwa wasanii wakubwa kutumbuiza na kuwajumuisha pia wasanii wa Uganda.

## Enock Bella akumbuka machungu

MSANII wa Bongo Fleva, Enock Bella, ambaye kwa muda mrefu amekuwa kimya, ameibuka na kudai amepitia mengi magumu baada ya kuvunjika kwa kundi la Yamoto Bendi.

Bella ambaye amerudi upya na mradi wake wa kuanzisha bendi ya muziki, amesema ilifikia kipindi alishindwa kulipia kodi ya nyumba na kumfanya kukimbia Dar na kwenda nje ya mji kujitafutia maisha.

Amesema ushirikiano kutoka kwa wasanii wenzie aliokuwa nao Yamoto umekuwa hafifu, lakini ameeleza urafiki wao uko sawa.





## HARMONIZE ANAPOSIFIA 'MORNING CALL'

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Harmonize amewafunga midomo watu wanaomkosoa kutokana na matumizi ya lugha ya Kingereza katika nyimbo zake, baada ya kupakua wimbo mpya 'Morning Call' ambao ameuimba kwa kutumia lugha hiyo pekee.

Awali Harmonize, alitoa kibao cha Single Again ambacho alikiandika kwa kimombo na kufanya vizuri zaidi kwenye majukwaa mengi ya kidijitali ya kupakua miziki ndani ya nje ya Afrika.

Jana asubuhi Harmonize aliachia ngoma hiyo kwenye mtandao wake wa YouTube, japo bado hakuachia video yake, mapokezi yamekuwa makubwa kutoka kwa wafuasi wake wasiochoka kumpa shavu.

FILAMU

## Catherine: Shemeji shemeji huku mwazima taa

**Na Adam Fungamwango**

UMDHANIAYE ndiye kumbe siye. Na umdhaniaye siye kumbe ndiye.

Unaweza kupata matatizo au mkasa ambao hujui chanzo chake ni nini.

Wakati mwingine anaweza kuwa ni ndugu ya damu ndiyo anakuumiza.

Filamu ya 'Catherine' inaweza kuwa mfano tosha wa haya ninayobainisha hapa.

Filamu hii imechezwa na magwiji wa tasnia hiyo nchini kama Hemed Suleiman, Jackline Wolper, msanii Najma Dattan, pamoja na msanii wa bongo fleva Hamad Ally 'Madee'.

Hemed anatokea kumpenda Najma ambaye ni dada wa Madee, huku wao wenyewe wakiwa ni marafiki wa damu.

Hata hivyo, Madee anapinga rafiki yake Hemed kumpenda dada 'ake kwa madai kuwa hajatulia.

Hemed anamhakikishia Madee kuwa ni kweli amekuwa kicheche, lakini kwa Najma atatulia na hatimaye kuoa kabisa na wala hana nia ya kumchezea, kitu ambacho kinapingwa vikali na rafiki yake huyo.

Mapenzi ya Hemed na Najma yanakuwa motomoto kiasi cha kwamba hakuna tena mtu wa kuyazuia kiasi cha kufikia posa kutolewa.

Kabla ya ndoa anawasili kutoka nchini Marekani alikokwenda kwa masomo dada wa Najma ambaye ni Wolper aliyecheza kama Sharon.

Aina yake ya maisha akawa anajijua mwenyewe, kwani ni tofauti na Najma ambaye amelelewa katika mazingira ya kumcha Mungu.

Sharon, binti aliyeishi kwenye nchi za watu, mwenye kuyajua ya usiku na ya mchana anaanza kuona wivu mdogo wake kuwa na mvulana 'handsome'.

Anatumia kila aina ya hila ili kumgombanisha Najma na Hemed na anafanikiwa.

Anamtumia kijana mmoja 'kumpaka' Najma mbele ya mchumba wake kuwa amekuwa akitembea na mume wa dada yake kiasi kwamba amesababisha dada yake kukosa amani kwenye ndoa.

Pia kijana huyo anatuma meseji za mapenzi kwenye simu ya Najma kwa kutumiwa na Sharon.

Hemed anachukia na kuachana na mchumba wake, lakini pia akiingia kwenye penzi la siri na dada wa mchumba wake Sharon. Shemeji shemeji kumbe wanazima taa.

Za mwizi arobaini, Najma anawafuma 'live' kitandani dada yake na mchumba 'ake kitu ambacho kinasababisha achanganyikiwe na kukimbia mbio kiasi cha kugongwa na gari, akajeruhiwa.

Sharon naye baada ya kuona hila zake zimegundulika anaamua kunywa vidonge kwa ajili ya kujiua, lakini anapona.

Kikao kikubwa kinafanyika na kila kitu kinagundulika.

Filamu inaisha kwa Hemed kufunga ndoa na Najma.







## Ali Kiba unaleta ubabe

TUKIO la Mwanamuziki wa Bongo Fleva. Alikiba kuonekana akiwa amewekа kitu kinachohisiwa ni silaha ya aina ya bastola, kwenye mfuko nyuma ya suruali yake imezidi kuibua sura mpya baada ya baadhi ya watu kudai ni tabia ya vitisho.

Hata hivyo, Kiba amekana kubeba silaha hiyo akidai kwamba kitu hicho ambacho kimesambaa katika mitandao ya kijamii kuwa ni Speedlight ya camera.

Watu waliotoa maoni yao wamesema wana uhakika msanii huyo alikuwa amebeba silaha nje nje jambo ambalo linatafsriwa kama ubabe na vitisho kwa wengine.

"Unapokuwa na silaha hutakiwi kuweka kama kitu cha mapambo. Suala hilo linatafsiriwa kama tabia ya vitisho na ubabe jambo ambalo si sahihi kwa watu maarufu kama yeye.

## DUNIA NI HII HII, WAENDAO VIUMBE

**Na Adam Fungamwango**

UKISIKILIZA hadithi nyingi na mambo mengi ya zamani na hata ukisoma kwenye vitabu mbalimbali vyenye kuheshimika, utagundua hakuna kitu kipya hapa duniani kinachofanyika.

Yote ni yale yale tu. Ni kama vile wanasayansi wanavyosema dunia inajizungusha yenyewe kwenye mhimili wake na kweli yote yanayofanyika yanajirudia tu.

Tena kuna vitu vingine vilifanyika zamani hadi leo hii havijafanyika tena. Vinavyoendelea kujirudia ni baadhi ya mambo machache tu yaliyofanyika miaka milioni nyingi huko nyuma.

Ndiyo maana utasikia watu wanakwambia maisha ya sasa ni magumu. Lakini ukisikia nyimbo za miaka 50 nyuma, utakuta wanaimba maisha ya sasa ni magumu. Ina maana yalianza kuwa magumu tangu zamani. Hivi sasa kuna udanganyifu wa mapenzi. Ukisoma vitabu vya miaka mingi nyuma, utakuta pia kulikuwa na udanganyifu.

Leo mada hii tutaziangalia nyimbo ambazo zinazungumzia dunia, raha, matatizo yake na vituko zilizotungwa miaka ya 1980 mwanzoni hadi mwishoni.

**Dunia Duara-Shaaban Dede**

Shaaban Dede akiwa na Bima Lee, alitunga kibao cha 'Dunia Duara'. Hiki kinazungumzia juu ya mtu anayechekwa na wenzake kuwa hana kitu.

Lakini mwenyewe anajipa matumaini kuwa dunia ni duara na huzunguka, hivyo anajua kesho atapata kwa jinsi anavyojituma. Anasema jua halina mpaka, huangaza pote kwa hiyo ipo siku na yeye ataangaziwa, kwani kama samaki baharini, wadudu mapangoni na wanyama porini wanaishi, basi kwa kudra za Mungu na yeye atapata tu.

**Dunia Uwanja wa Fujo-Marijani**

Jabali la Muziki Marijani Rajab, yeye akatunga kibao cha 'Dunia Uwanja wa Fujo'. Anawatahadharisha wote wanaojimwambafai na kuiona dunia kama yao, kuwa walikuwepo watemi, wafalme wenye nguvu, lakini leo hii hawapo.

Alikuwepo Firauni, Hitler, Nduli Idd Amini ambao historia inasema ni moja kati ya viongozi wababe kuwahi kutokea duniani, lakini kwenye dunia hii hakuna mbabe kushinda Mwenyezi Mungu.

Kwa maana hiyo anawaasa watu hususan wanaopewa dhamana, kuishi vizuri na watu, kwa sababu ubabe hauna maana akamalizika kwa kusema kwenye dunia hii 'kula ugali wako ukalale'.

**Dunia-Remmy Ongalla**

Remmy Ongalla kwenye fasihi yake ya wimbo huu wa 'Dunia' anasema yote ambayo binadamu atakayofanya hapa duniani, ikiwa ubaya au wema, atalipwa hapa hapa ulimwenguni.

Anasema kwa Mungu hatupajui, hivyo binadamu anatakiwa kutenda wema, kwani kuna baadhi ya watu hudhulumu wengine kwa vyeo vyao, wadhifa, pesa na umaarufu.

**Dunia-TX Moshi William**

Akiwa na bendi ya Polisi Jazz, kabla ya kujiunga bendi ya Juwata Jazz, alitunga kibao kisemacho 'Dunia'. Anauliza, mwezi na nyota usiku zinang'aa bili yake analipa nani? Na ilitakiwa kabisa aulizwe anayelipwa bili ni nani? Huyo ni mwenyezi Mungu. Yeye kila kitu hutoa bure kwa waja wake.

**Dunia Imani Imekwisha-Marijani**

Hapa Marijani amerudi tena hapa na wimbo wa 'Dunia Imeni Imekwisha'. Yoyote aliyedhani eti sasa ndiyo kuna dhana hiyo, lakini hata miaka ya 1970 hadi 1980, kulikuwa na matendo kiasi cha kuonekana dunia imani yake ni ndogo. Watu wanaibiana. Wanatapeliana. Wanadhulimiana. Kuna wanaodhulumu watoto yatima. Wanaotaka kuwaua wazazi wao ili warithi mali na mengine mengi.



# Lil Wayne, Nicki Minaj wana jambo

Imekuwa ni wiki ya wasanii wawili Nicki Minaj kutoka Trinidad and Tobago na rapa wa Kimarekani Lil Wayne kusifiana, kila mmoja akimfagilia mwenzake, mpaka baadhi ya watu wanajiuliza, "au kuna namna?"

Akiwa na wachezaji wa zamani wa NBA, Matt Barnes na Stephen Jackson, rapa huyo alimmiminia misifa mwimbaji huyo wa kike akisema

"Hakuna mtu anayecheza na Nicki, wengine wanafuata," alisema rapa huyo.

"Tulikuwa tunatafuta wasanii wakati huo na tukajipanga kutafuta wasanii wa kike New York na nilipomsikia, Nicki alikuwa anasikika kama mimi na alikuwa akibadilisha sauti yake juu, nilisema kamwe sijawahi ona kipaji kama hiki, na hii ni nadra sana," alisema.



## Davido kumbe ana mtoto mwingine

MWANAMUZIKI mkali kutoka Nigeria, Davido, amethibitisha kuwa na mtoto wa kiume, anayeitwa Dawson, ambaye amezaliwa na mrembo Larissa.

Msanii huyo alizungumza kuhusu mtoto huyo, kwenye kipindi maarufu cha AB Talks, amesema mtoto huyo atakuwa wanne ambao anawafahamu.

"Niliwaita binti zangu wote wawili kwa jina la mama yangu. Binti yangu wa pili ni kama mama yangu. Ni kichaa. Nina mtoto wa kiume pia, anaitwa Dawson ambaye anaishi London hivi sasa."

## Lanez imekuwaje ukatwanga mrembo risasi?

Rapa na mwimbaji raia wa Canada, Tory Lanez amehukumiwa kwenda jela miaka 22 na miezi minane, baada ya kupatikana na hatia ya kumtwanga risasi mwimbaji wa kike Megan Thee Stallion raia wa Kimarekani.

Tory Lanez ambaye jina lake halisi ni Daystar Shemuel Shua Peterson, amehukumiwa Los Angeles nchini Marekani wiki hii, kwa kumpiga risasi na kumjeruhi msanii huyo wa hip hop ambaye naye jina lake halisi ni Megan Jovon Ruth Pete.

Rapa huyo alipatikana na hatia Desemba 23 mwaka jana, lakini hukumu ilicheleweshwa baada ya kupata mawakili wapya ambao waliwasilisha ombi la kesi hiyo kuanza upya.





## Adui filamu Marvel hapatoshi

Mcheza filamu Tenoch Huerta raia wa Mexico amekanusha madai ya kumnyanyasa kijinsia mchumba wake wa zamani, mwanamuziki na mwanaharakati Maria Elena Rios.

Huerta, aliyecheza kama adui, au mhalifu mkuu kwenye filamu ya Marvel, alikanusha hayo baada ya mpenzi wake huyo kudai kuwa amekuwa akinyanyaswa kijinsia na dear x wake huyo katika mtandao wa twitter kwa siku za hivi karibuni.

"Takriban mwaka mmoja uliopita nilichumbiana na Elena kwa miezi kadhaa, ilikuwa ni makubaliano wakati wote, kama wengine wengi wanaweza kuthibitisha, na wakati wote ulikuwa uhusiano wa upendo, na wa kusaidiana na hata baada ya kuachana," alisema nyota huyo aliyecheza pia filamu ya Black Panther.

## Mtoto wa 2 Chainz hautaki utajiri

Mtoto wa pili wa rapa wa Kimarekani 2 Chainz ameweka wazi kuwa havutiwi na utajiri wa baba yake, lakini anampenda kama mzazi wake.

Mtoto huyo ambaye jina lake ni Halo, alisema hayo katika mahojiano mafupi aliyofanya na 'clip' yake kurushwa kwenye mitandao, alikiri kuwa kweli baba yake ni tajiri, lakini kwake anampenda kama baba na havutiwi na utajiri wake, anaona poa tu.

Issa Rae ambaye ndiye alikuwa akimhoji alianza kwa kumuuliza

"Unajua baba yako ni nani?" Halo akajibu, "Ndiyo. 2 Chainz." "Yeye ni nani kwako?" Rae akauliza tena.

"Baba yangu ni mtu tajiri tu ndani ya nyumba, namaanisha huyo ndiye baba yangu."

Alipoulizwa kama anavutiwa na hilo, baba yake akajibu "Pesa zangu ni pesa zako pia."







Mfamasia kutoka ofisi ya Mganga Mkuu Hospitali ya Wilaya ya Mkinga, Jonas Mbwambo akitoa elimu kwa madereva bodaboda kuhusu matumizi sahihi ya dawa jana, kupitia wiki ya famasia amesema wanaadhimisha wiki hiyo kwa kutoa elimu kwa jamii katika maeneo yao. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# CAG kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi Babati

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amesema wakati wowote kuanzia sasa atatua katika Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara, kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi ili kujiridhisha juu ya mamilioni ya shilingi yanayotajwa kutafunwa katika halmashauri hiyo.

Alitoa ahadi hiyo juzi wakati akizungumza na madiwani wa halmashauri hiyo waliokutana kujadili taarifa za CAG kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

"Ukaguzi huu siyo wa kumwondoa mtu, ni kujiridhisha ili kubaini waliohusika kusababisha hoja za ukaguzi. Kila aliyehusika atajulikana, awe mwanasiasa au mtaalamu wa halmashauri atajulikana katika ukaguzi huu wa uchunguzi.

"Nimeamua kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi na siyo ukaguzi maalumu kama alivyoomba Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, baada ya kuona halmashauri hii ina upungufu mkubwa wa kutafuna fedha za umma," alisema Kichere.

Alisema kuwa ameamua kufika yeye mwenyewe katika halmashauri hiyo ili aone ni kwa namna gani halmashauri inapata hati yenye shaka katika ukaguzi, kwa kuwa alipokuwa akipokea ripoti kutoka kwa wasaidizi wake, alikuwa anatia shaka.

Alisema hata wasaidizi wake wanapokuwa wanafanya ukaguzi wananyimwa ushirikiano na nyaraka zinazokuwa zinatakiwa hawapewi na hupatikana wakiwa tayari wameshaondoka.

"Hamtutendei haki kutokutoa nyaraka na tunakuwa na wasiwasi na nyaraka zinazotolewa kwa kuchelewa wakati mwingine tunaweza kusema nyaraka zimetengenezwa,"alieleza.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, akizungumza katika kikao hicho, alisema hati ya shaka waliyoipata halmashauri hiyo haijamridhisha na haijambariki.

Sendiga aliagiza watendaji waliosababisha kupata hati yenye shaka wachukuliwe hatua. Alisema hal-

# EALA, asasi za kiraia wajadili utatuzi vikwazo vya biashara

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

KAMATI ya Kudumu ya Mawasiliano, Biashara na Uwekezaji ya Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), imekutana na kufanya majadiliano na mwavuli wa asasi za kiraia wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo ili kutafuta suluhu ya baadhi ya vikwazo vya kibiashara vinavyofifisha utangamano kupitia sekta hiyo.

Juzi Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Suleiman Shaban, kutoka nchini Kenya, alisema kikao kazi hicho kinalenga pia kutizama vipi watafanya kazi pamoja ili kuboresha uhusiano wa kibiashara wa kijamii na wa kisiasa katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC).

"Kamati ya EALA, tulikuwa na majadiliano na kubadilishana mawazo na asasi za kiraia. EALA tumebaini kuna mambo mengi kwenye biashara ambazo zinatokea mara nyingi na tunafikiri kama tusipokaa pamoja tukatafuta suluhisho kwa hayo masuala ya kibiashara, mambo yatakuwa magumu zimekuwa zaidi.

"Ndio sababu tukaamua tukutane kama EALA na hizi asasi za kiraia ili tutafute njia za kuleta suluhisho. Hivi sasa kuna shida nyingi za kibiashara, lakini tunaamini kwamba hakuna shida ambayo haina suluhisho.

Zaidi aliongeza: "Tukikaa tukibadilishana mawazo, tukibadilishana fikra tutapata suluhisho. Nia yetu ni kuleta uhusiano mwema na utengamano wa kisiasa. Washiriki wa mkutano huu wanatoka Uganda, Tanzania, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini na Kenya."

Mkurugenzi wa Mwavuli wa Asasi za Kiraia wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACSOF), Lilian Alex, alisema ili kuja na mkakati wa pamoja wamekubaliana kufanya mkutano mkuu wa Jukwaa la Mwaka la Asasi za Kiraia (EACSOF).

"EACSOF ni mwamvuli unaoziweka pamoja asasi za kiraia kutoka nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Majadiliano tuliyoyafanya tunatazamia sisi kama asasi za kiraia, yatakuja na suluhisho la utatuzi wa matatizo mbalimbali.

"Kimsingi tunakabiliwa na vikwazo vya kibiashara, kwa hiyo sasa tunaangalia ni jinsi gani nchi wanachama wanaweza kuzitatua kupitia wizara zao za mambo ya nje, pale zinapokutana. Tumefurahi kusikia kwamba angalau kwa mwaka huu tunaweza jukwaa la mwaka la asasi za kiraia. Ni jukwaa ambalo linaleta pamoja asasi za kiraia, sekta binafsi pamoja na serikali za Jumuiya ya Afrika Mashariki."

Mkurugenzi wa asasi ya kiraia ya SIATIN, Jane Narunga, alisema mambo mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na kutengeneza fursa za kuwaleta pamoja wawakilishi au wabunge wa EAC na nchi wanachama.

Pia alisema liko suala zima la utatuzi wa kodi zinazotozwa katika mipaka kutokana na usafirishwaji wa mizigo, kwamba katika hilo asasi za kiraia zinatafuta ni jinsi gani zinaweza kuingia na kufanya kazi na serikali za nchi mbalimbali katika kusaidia kutatua tatizo hilo la muda mrefu la kukuza biashara.

## BAKWATA yaishauri taasisi kuwekeza miradi ya jamii

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SHEKHE Mkuu wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Mkoa wa Kilimanjaro, Shaban Mlewa, ameishauri Taasisi ya Al Atar A' Charitable Foundation (ACF) na Quatar Charity, kujikita zaidi kuwekeza miradi yake ya jamii, hasa ujenzi wa zahanati kwenye maeneo ya pembezoni yenye uhitaji mkubwa.

Alitoa ushauri huo juzi alipopewa nafasi ya kuzungumza na wananchi wa Kijiji cha Kalimaji kilichoko Kata ya Mitimirefu, Wilaya ya Siha wakati wa hafla ya makabidhiano ya zahanati iliyojengwa na taasisi hiyo.

"Wilaya ya Siha bado ni changa na ina mahitaji tofauti na wilaya nyingine ambazo zina miundombinu ya kutosha. Huku bado mazingira yenyewe yana uhitaji, watu ni wengi; kwa hiyo kama wamefanya hili, pia wasisahau kufanya jingine. Tunawashukuru kwa kutujengea zahanati hii, lakini tunaomba watusaidie kujenga na nyumba ya daktari.

"Kuna Kata ya Kashashi, nayo inahitaji kubwa la zahanati kama hii, kwa hiyo inapotokea fursa wasikimbilie mijini sana, AL ATAR 'A wakimbilie watu wa vijijini. Hawa watawaombea kwa dhati, maana kule mjini wanaweza wakajenga lakini wakatahamaki hospitali ziko mikononi mwa watu wananufaika na fedha na vitu vinginevyo."

Kabla ya makabidhiano hayo, Ofisa Uhusiano wa Taasisi ya Al Atar A' Charitable Foundation, Abubakar Rajab, alisema ujenzi wa mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 100 hadi kukamilika kwake.

"Ujenzi huu wa Zahanati ya Kalimaji, tulizungumza na Wizara ya Afya, kwa maana ya Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, ambaye alituelekeza ijengwe hapa Kalimaji.

"Kimsingi, ujenzi wa zahanati hii kuanzia majengo, samani za ofisi na vifaa tiba vyote thamani yake ni zaidi ya Sh. milioni 100. Tunategemea kadri mji unavyokua, serikali inatabia ya kufanya uendelezaji wa miradi, hivyo zahanati hii tunaamini kwamba itaongezewa majengo," alisema. Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kalimaji, Zainab Ally, alisema: "Kupata zahanati hapa tunamshukuru Mungu sana. Tunawapongeza hawa wenzetu walioguswa na shida yetu na kutusogezea huduma za afya. Huku kuna wanyamapori wakali wanazunguka vijijini na ikitokea usiku mtu anahitaji huduma za afya, inabidi akodi gari na kama huwezi itabidi usubiri asubuhi. Tembo ni wengi na ndiyo tishio kubwa kwetu."

Aidha, Yohana Yaro, mkazi wa Kijiji cha Kalimaji, Kata ya Miti Mirefu, alisema kujengwa kwa mradi huo ni hatua moja ya kuwafuta machozi.

"Tumeteseka sana kufuata huduma za afya wilaya jirani ya Longido na mara nyingine tunalazimika kwenda Sanya Juu iliko Hospitali ya Wilaya ya Siha, ambapo saa nyingine wake zetu, mama zetu labda anataka kujifungua kwa operesheni inashindikana inabidi uende Hospitali ya Wilaya. Nauli tunayotumia kutoka Kalimaji kwenda Sanya Juu, siku kuna usafiri wa mabasi madogo nauli ni Shilingi 8,000 kwenda na kurudi lakini wale wanaokodisha pikipiki ni Shilingi 15,000 kwenda Sanya Juu kwa hiyo kwenda na kurudi ni Shilingi 30,000. Huko Longido ni Shilingi 30,000," alisema.

Baada ya makabidhaino hayo, Diwani wa Miti Mirefu, Simon Shija, aliwashukuru wahisani hao akisema awali kwenye kata hiyo kulikuwa kuna shida ya afya.

Alisema zahanati waliokuwa wanaitumia kwa huduma iko Wilaya ya Longido (Arusha) na upande mwingine walikuwa wanakwenda kilomita zaidi ya 14 kupata huduma za afya, Kata ya Ngarenairobi na Sanya Juu.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Mihogo ya kukaanga inavyotamba miaka nenda rudi

## -Haichuji nyumbani, ofisini, shuleni ndiyo balaa

**Na Adam Fungamwango**



HAPANA shaka msomaji yeyote atakubaliana na mimi kuwa mihogo ya kukaanga ndiyo chakula cha muda wote kuliko vingine, inavyoliwa na watu wa rika zote, tangu enzi na enzi.

Hata mzee wa miaka 90, atakuambia kuwa wakati anasoma shule walikuwa wakila mihogo ya kukaanga akiwa shuleni. Na hadi leo atakuambia bado anakula na anaipenda.

Wengi wetu tumekula mihogo ya kukaanga kuanzia shule ua msingi, sekondari na hata tulivyokuwa vyuoni. Hiki ni chakula cha kuma mrefu zaidi kuliwa na watu wa maisha ya kawaida.

Najua kuna vitumbua, maandazi, egg chop, katless, visheti, kalimati, bagia, chapati, mikate ya kumimina, lakini ni kama vile vyakula hivi vinakuja na kuondoka, mihogo ya kukaanga inabaki pale pale na ubora wake.

Kinachoitofautisha mihogo na vyakula vingine ni kwamba inaliwa popote pale, shuleni, vyuoni, mtaani, maofisini, majumbani na watu wa aina zote.

Wapo wanaoona kama mihogo hasa ya kukaanga inakuwa zaidi na watu wa hali ya chini, lakini ukweli hauko hivyo. Inaliwa hata mabosi, unajua sababu yake?

Ni kwamba hata hao mabosi walikuwa wanafunzi zamani na walikuwa wanaila shuleni, hivyo hata akiwa amevaa suti yake, ataitamani tu. labda atakachofanya ni kumtuma mesenja kwenda kununua. Ataila hata kwa hamu tu, na si kwamba hana pesa, au anaila kwa njaa, la hasha.

Uzuri wa mihogo ya kukaanga ni kwamba haikinahi, kuna siku inaweza kuliwa kwa njaa ili kupitisha siku na inaweza kuliwa hata kwa hamu tu, kama vile mtu anayekula karanga, au korosho.



Kinachotofautisha, ni kwamba zamani kwenye miaka ya 1970 mpaka 1980, hakukuwa na chachandu, au kachumbari mashuleni, badala yake kulikuwa na pilipili ya unga ilikuwa imechanganywa na chumvi.

Waliosoma miaka hiyo wanalijua hili.

Unakwenda kununua muhogo, unawekewa kwenye karatasi, wakati huo hakukuwa hawakuwa wanaweza kwenye vyombo kama sahani au mabakuli kwa sababu hata nyumbani tu ilikuwa inshu kupata hitu hivyo, unatiliwa chumvi mhanganyiko na pilipili ya unga, mambo yanakwenda. Unakunywa maji, masomo, kengele ikigongwa unakwenda kuendelea na masomo.

Kachumbari zilianza kutengenezwa mwishoni mwa miaka ya 1980 na 1990, lakini wanafunzi walikuwa hawafaidi sana kwa sababu bado walikuwa wanafungiwa kwenye makaratasi. Hata mitaani ilikuwa ni hivyo hivyo.



Wala mihogo wa kukaanga, hususan wanafunzi walianza kufaidi utamu wa kachumbari, vyombo vya plastiki vilipoanza kuwa vingi nchini na watu kumudu kuvinunua, hapo sasa walaji wakiwemo wanafunzi walipata utamu halisi wa mihogo na kachumbari kwa sababu mchuzi unabakiwa kwenye bakuli kabla ya kunywewa na mnunuaji.

Ila tu kuna wakati unaweza kukutana na mchuzi ya nyanya iliyooza. hiyo ni siri yako.

Mpaka sasa, biashara ya mihogo ya kukaanga inaendelea kushamiri na kushamini. Inaonekana haipitwi na wakati, achilia mbali wateja wake wengi kuwa wanafunzi, lakini miaka ya karibuni imekuwa ni kama kitafunio cha chai kwa familia nyingi hasa mikoa ya Pwani, hususan jijini Dar es Salaam.

Mihogo ya kukaanga sehemu nyingine inashika nafasi ya pili kwa kuliwa ikitanguliwa na chips, kwani watu wananyea chai, maji, juisi na hata samaki wa kukaanga.

Wafanyabiashara nao wamejiongeza kwa sababu mihogo ya kukaanga ina kitu kinaitwa chachandu. Ni aina ya siki hivi, ambayo ni mchanganyiko wa kiungo mbalimbali kama mbilimbi, ndimu, ukwaju, pilipili, nyanya na vikorombwezo vingine, hivyo kuongeza utamu kwa mihogo hiyo.

Kama kawaida, mada hii iliwekwa mtandaoni na baadhi ya wasomaji walileta mrejesho kwa jinsi walivyokumbuka mihogo ya kukaanga enzi hizo wakiwa shuleni.

"Mwe umenikumbusha pale Mgulani Primary, mihogo na 'ice cream,' ndiyo zangu, hela yangu ya shule mara nyingi huishia hapo." Aliandika msomaji mmoja. Mwingine akaandika maneno yafuatayo.

"Tuliila sana shuleni, lakini mpaka sasa ni chakula ambacho unaweza kuila muda wowote, kwa chai, maji na hata juisi na hata ukipata samaki wakukaanga hunoga mno. Na sio lazima uwe na kachumbari waweza kula na tomato, chili sio mbaya."

"Kila aliyepitia shule za msingi, sekondari, anajua utamu wa mihogo ya kukaanga na chachandu, masalo, nyanya za kuoza." Akaandika msomaji mwingine.

"Kuna aina fulani ya maisha tunayaendea huko mbele tukiishi kwa kuangalia watu watatuonaje maisha yatakua magumu mno, mtu eti anaona aibu kula mihogo ya kukaanga anadhani ataonekana ni masikini wakati tuliila tangu tukiwa shuleni," aliandika mama mmoja akichangia mada.

"Katika jiji la Dar mihogo ya kukaanga siku hizi imekuwa kama ndiyo chakula kikuu katika maeneo mengi ya jiji, kila ukizunguka utakuta muuzaji na watu wanakula.

Kuna watu anasema pengine ni ugumu wa maisha, lakini wengine wanasema ni kubadilika kwa mfumo wa maisha, watu wengi wameshaanza kujua vyakula vinavyorutubisha mwili na si kula chanye utamu mdomoni, ndiyo maana hata mabosi na wenye pesa bao tunawaona wananunua mihogo ya kukaanga.

**Tuma meseji 0716 350534**

# YST yataka mifumo ya elimu iboreshwe

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKISHO la Wanasayansi Chipukizi (YST) limeiomba serikali kuboresha mifumo ya elimu itakayowezesha wanafunzi kushiriki katika mapinduzi ya viwanda.

Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha, alitoa rai hiyo juzi alipozungumzia maonyesho ya wanafunzi chipukizi ya sayansi ya kibunifu na kigunduzi ambayo hufanyika kila mwaka.

Dk. Kamugisha alisema dunia imeingia katika mapinduzi ya nne ya viwanda, hivyo Tanzania haipaswi kuwa mtazamaji bali mshiriki imara wa mapinduzi hayo ikiwamo kuhakikisha miundombinu na mifumo ya elimu inaboreshwa kuwezesha wanafunzi kujiingiza katika eneo hilo. Alisema ni muhimu Tanzania nayo ikajiandaa kwa mapinduzi hayo yaliyojikita katika matumizi makubwa ya teknolojia.

"Kadri Tanzania inavyoelekea katika mapinduzi ya nne ya viwanda, YST nayo imefanya juhudi za kuwandaa vijana wanaosoma shule za sekondari kuwa washiriki imara wa mapinduzi hayo kwa kuboresha ujuzi wa kisayansi na teknolojia kwa vijana," alisema Dk. Kamugusha.

Alisema kupitia mpango wa mafunzo shuleni, YST imekuwa ikiwapatia vijana ujuzi wa kubaini matatizo ya kimaendeleo katika jamii zao na kubuni njia mbalimbali za kisayansi kukabiliana na matatizo hayo katika muktadha wa mapinduzi ya nne ya viwanda.

Kuhusu maonyesho ya wanasayansi chipukizi, alisema wanafunzi hao watapata fursa ya kuonyesha kazi zao za kiteknolojia katika maonyesho yanayotarajiwa kufanyika Desemba mwaka huu.

Alisema kazi za sayansi na teknolojia ambazo kwa sasa wanafunzi wanaendelea kuzifanyika utafiti, zimejikita katika nyanja mbalimbali za kisayansi na teknolojia na kwa mwaka huu maombi ya kazi za kisayansi 979 yamepokewa na YST kutoka kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Alisema kazi hizo za kisayansi zinajumuisha matumizi ya mifumo ya umwagiliaji kupunguza upotevu wa maji na kufanya mtawanyiko sawia wa virutubisho vya mimea katika udongo, virutubisho vya kibaiolojia kuzuia udumavu wa mimea na njia za kupunguza madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Kiongozi huyo alisema kazi nyingine zitakazoonyeshwa ni za njia salama za usafirishaji maji na za kugundua upotevu wa maji kwa kutumia sensa.

Ofisa Mtendaji wa Taasisi ya Karimjee (KJF), Caren Rowland, alisema kazi za kisayansi zinazofanywa na wanasayansi chipukizi ni za kipekee ambazo zimekuwa chachu ya masomo ya sayansi shuleni.

Caren alisema YST imekuwa msaada mkubwa katika kukuza sayansi nchini kwa wanafunzi na kwa walimu pia.

# Watuhumiwa wizi Mil. 47/- za Tanzanite kupandishwa kizimbani

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WATU wawili waliokamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Manyara kwa tuhuma ya kuvunja nyumba na kuiba Sh. milioni 47, wanatarajia kufikishwa mahakamani Jumatatu.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Kamishna Msaidizi wa Polisi George Katabazi, alisema jana kuwa watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa katika viunga vya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Juma Athuman (23) na Mariam Mbega (26), wote wakazi wa Mirerani.

Kwa mujibu wa Katabazi, watuhumiwa hao wanadaiwa walivunja nyumba na kuiba fedha hizo ambazo ni mali ya mfanyabiashara na mkazi wa eneo hilo, Lawrent Elias.

"Polisi waliwafuatilia watuhumiwa hao hadi Wilaya ya Handeni mkoani Tanga na jijini Dar es Salaam na kuwakamata. Hivi sasa wanashikiliwa katika Kituo cha Polisi Mirerani na Jumatatu mapema iwezekanavyo tutawafikisha mahakamani Simanjiro," alisema.

Baada ya kukamatwa kwa watuhumiwa hao, mfanyabiashara huyo (Elias) ambaye kitaaluma ni mlipuaji miamba ya madini ya Tanzanite, alipongeza Jeshi la Polisi kwa kufanikisha kuwakamata kwa kuwa limeonyesha juhudi kubwa na uadilifu wa hali ya juu.

"Ninamshukuru Mkuu wa Jeshi Polisi, IGP Camilius Wambura, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara (Katabazi) na Mkuu wa Kituo cha Polisi Mirerani (Dominick Fwaja) kwa kufanikisha suala hili," alisema Elias. Alidai Jeshi la Polisi linastahili pongezi nyingi kwa kuwa baada ya uhalifu huo, watuhumiwa walizificha fedha hizo benki.

"Polisi wamezuia akaunti inayomiliki fedha hizo, zisitoke wala kuingia benki ili utaratibu wa kisheria ufuatwe katika tukio ambalo lilitokea Juni 6, 2023 katika Mji Mdogo wa Mirerani," alisema.

Pia alitoa ufafanuzi kuhusu kuwa na fedha nyingi kiasi hicho nyumbani badala ya kuweka benki, akisema ni kutokana na usalama ulioko nyumbani kwake.

"Kwa ukanda huu kuwa na fedha nyingi siyo jambo la ajabu kwa kuwa fedha za mkononi unaweza kununua bidhaa kama madini kwa urahisi kuliko kuwa na fedha benki, hivyo biashara kukupita," alisema.

Alidai kuwa mbali ya fedha, watuhumiwa waliiba simu mbili ndogo na kurunzi (tochi) ambazo pia polisi walikamata na vielelezo hivyo. Viko polisi.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo kulia akiwa na Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Lindi, Hassan Jarufu, Wapili Kulia juzi wakizindua zoezi la ugawaji pembejeo za kilimo zilizotolewa bure na Rais Samia Suluhu kwa wakulima wote wa Nachingwea. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# 'Bidhaa hatarishi zidhibitiwe badala ya kuziongezea kodi'

**Na Beatrice Shayo**

WADAU wa mazingira wameishauri serikali kudhibiti uingizaji wa 'bidhaa taka', hasa zinazotoka mataifa ya Ulaya na Amerika, badala ya kuongeza kodi kwa kuwa zimekuwa zikiharibu mazingira.

Jijini Dar es Salaam jana, Mtaalamu Mwekezaji wa Masuala ya Mazingira kutoka Taasisi ya Jielimishe Kwanza, Henry Kazula, alitoa rai hiyo, akisema taka hizo hutoka katika nchi zinazoendelea ambazo ni bidhaa za kielektroniki na nguo zinaingia nchini kwa jicho la msaada.

Kazula alisema kuwa katikam masoko, wamebaini baadhi ya bidhaa zimeingizwa nchini mithili ya taka zinazopelekwa dampo, jambo ambalo serikali inatakiwa kudhibiti ili kutunza mazingira.

"Kiatu kimekuja nchini kimeisha na huwezi kusema unakinunua. Hii imekuwa ni changamoto katika suala nzima la uhifadhi wa mazingira nchini kwa sababu bidhaa hizi kwa muda mfupi tunakuja kuzikuta katika maeneo yetu ya mazingira, hasa katika fukwe tunazikuta zimetupwa huko," alisema.

Mtaalamu huyo alisema wanaharakati mbalimbali wamekuwa wanapambana kusafisha fukwe, wanakutana na viroba vya viatu vilivyotumika na nguo za mitumba.

Kazula alisema wamefurahia ongezeko la kodi kwa vyombo vya usafiri ambavyo ni chakavu kwa mwaka ujao wa fedha. Litasaidia kupunguza hewa ukawa ambayo ni kichocheo cha mabadiliko ya tabianchi.

"Hii itakatisha tamaa watu kuagiza vyombo vya moto chakavu. Wataagiza vilivyo bora maana maeneo mengi ya mjini yataonekana kama ni sehemu ya dampo endapo hapatakuwa na udhibiti," alisema.

Pia alisema fedha zinazotengwa na serikali kwa ajili ya mazingira ziwe zinashuka kwa wadau ambao wanachangia juhudi za uhifadhi wa mazingira.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Manispaa ya Temeke, Linda Munisi, alisema taka hizo ambazo huingia nchini zinaharibu hali ya hewa. Zinajumuisha magari yaliyotumika ambayo hayafai.

"Haya magari yanapongia nchini yanatoa hewa chafu ambayo inasababisha kuharibu hewa, mwisho wa siku mtu anapata magonjwa ya saratani ya mapafu. Taka hatarishi ni nyingi ambazo zinaingia nchini zikiwamo simu na kompyuta," alisema.

Mshauri wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Hilaly Ballonzi, alisema kuna umuhimu wa kuzungumzia suala hilo ambalo lipo kwa muda mrefu.

"Niliuziwa kompyuta ambayo imetumika, nimeitumia miezi mitatu imezima. Nimepeleka kwa fundi ninaambiwa haifai kutengenezwa, wakanishauri nikanunue mpya. Hii haitengenezeki tena, sio tu kwenye athari za kimazingira hata za kiuchumi," alisema Ballonzi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**ODED GRADY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye majina ya umiliki **SISTA SAFARI COMPANY** yenye usajili namba: **T244 DKL, CHASSIS NAMBA: ACA210160100** na **ENGINE NAMBA:IAZ4187338.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/204404/202**

## KUPOTEA KWA PASPOTI YA KUSAFIRIA



**DANIEL SONGAMBELE MAPILYA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE289571** iliyotolewa makao makuu **DAR ES SALAAM PCO** mwaka **2020.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: IRI/IRI/RB/252535/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKA KUU DODOMA**
**MAOMBI MADOGO YA MADAI NA. 21 YA 2023**
**PASCHAL JOHN SENI.........MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**RASHID SEIF KILAMA**
**IBRAHIMU JUMA KASIKA**
**UNCLE MO ENTERPRISES............WAJIBU MAOMBI**

**KWA: IBRAHIM JUMA KASIKA,**
**POPOTE PALE ALIPO.**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA MAOMBI MADOGO YA MADAI**
**NA. 21/2023 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**
**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma, mbele ya MHE. S. S. LUSHASI, NAIBU MSAJILI wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya alhamisi tarehe 22/06/2023.
HIVYO; Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
NA ENDAPO; hautafika wewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.
IMETOLEWA; kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 08/06/2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU DODOMA

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPH HAULE,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha Ualimu cha daraja la tatu 'A' chenye Index namba **E 509-0202** kilichotolewa chuo cha Ualimu cha Songea mwaka 1997.
Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**TAARIFA YA POLISI SOG/RB/2831/2023.**

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**NENELWA J. MWIHAMBI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T843DUJ** aina ya, **RAV4.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/203918/2023.**

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**NENELWA J. MWIHAMBI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T843DUJ** aina ya, **RAV4.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/203918/2023.**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**
**CRIMINAL/MISC CIVIL APPEAL CASE/ MATR, CAUSE/ REV, PROB ADM**
**CASE NO. 14 OF 2023**
**HAWA SHABAN MAKUBI .....PLAINTIFF/APPELLANT**
**VERSUS**
**JITEN MAHESH SHAH.....DEFENDANT/RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE MENTIONED/HEARING**

THE NOTICE that the above case has been fixed for Mention/Hearing on 26 day of 06, 2023 at 9:00 am
Before Hon. T. KANIKI DRM
YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce to that day all the documents upon which you intend to reply in support of your case.
Given under my hand and the seal of the Court thi 14 day of 06 , 2023

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO

DISTRICT COURT
P. O Box 660, Morogoro

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL.**

BY THIS DEED, I BONIFACE WILSON MBULI OF P. O. Box 50 KIDATU DO HEREBY wholly, absolutely and utterly renounce, relinguish and abandon the the use of the former name of BONIFACE P. WILSON and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of the former name, the name of BONIFACE WILSOB MBULI for the purpose of evidanceof such determination, I, hereby DECLARE that hi will at all times hereinafter in all records, deed, documents and otherwriting and in all action, suits and proceedings as well as in all Publis and Private dealings and transactions and creations whatsover use and subscribe the said name of BONIFACE WILSON MBULI appear on my National Identification Card with No. 19671125-67508-0000-426 in lieu of and in submition for the former names of BONIFACE P. WILSON
AND I HEREBY expressly authorize and require all and every person and whatsover at all times after the date hereof to designeted describe and adress him by the adopted name of BONIFACE WILSON MBULI
IN WITNESS WHERE of I have set my hand at MOROGORO, and I hereon substitute the old name of BONIFACE P. WILSON by the new name BONIFACE WILSON MBULI

SIGNED and DELIVERED by the said BONIFACE WILSON MBULI

DEPONENT



BEFORE ME:
Signature:
Postal Address:
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-13

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Alipomaliza kuongea na afande huyo alichukua simu yake ya mkononi, akabonyeza vitufe na kuiweka sikioni.

"Niambie mtoto wewe umeshatoka ofisini?"

"Ndiyo si uliniambia nitoke."

"Ni kweli, sikutaka tuongeee maneno haya ukiwa ofisini, vipi umeshamaliza kazi?"

"Nimemaliza, nipo kwenye gari yangu narudi nyumbani sasa."

"Enhee kazi yangu umeniambia umeifanya, inasemaje?"

"Nimeifanya na nitakutumia kesho kwenye email yako, lakini kwa kifupi mtu uliyeniambia nifuatilie safari zake ni kwamba, mara zote safari zake ni za kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Kwa uchunguzi wangu mfupi tu ni kwamba huyu ni mtumishi wa umma, yaani ni mfanyakazi wa serikali. Inaonekana kwamba ana safari nyingi tu za Dar na Dodoma, lakini nyingine hatumii ndege, anatumia magari ya kawaida tu ya serikali, ila mara hizi ambazo ninakutumia kwenye mtandao anatumia usafiri wa ndege."

"Du, nadhani umeanza kunipita hata mimi mwenye kazi yangu." Eddy alitania. Maria akaangua kicheko.

"Umeona eee, inabidi uje uniajiri niwe nakusaidia." Akajibu na sasa ikawa zamu ya Eddy kucheka.

"Ni mara moja tu ambayo safari yake haikuwa ya Dar Dodoma au kutoka Dodoma kuja Dar."

"Alaa, alikwenda wapi?"

"Inaonekana alitoka Mwanza kuja Dar tu na kesho yake, akatoka Dar kwenda Dodoma."

"Katika safari hizo zote, ipo siku ambayo alitoka Dodoma kuja Dar, halafu kesho yake akarudi Dom?"

"Hapana Eddy, mwenyewe utaona kwenye email yako, safari zote huwa zinaachana. Inaonekana jamaa Dodoma ni kazini, halafu Dar ni nyumbani kwake. Dodoma hukaa wiki nzima, halafu Dar es Salaam siku mbili au tatu."

"Kwa maana hiyo ni siku ambayo alitoka Mwanza kuja Dar ndiyo alikaa kwa siku hiyo kesho yake akapanda ndege ya kwenda Dodoma?"

"Ni kweli."

"Vizuri, sasa hiyo emali utakayonitumia, niwekee mpaka muda ambao ameshuka siku hiyo alipotoka Mwanza kuja Dar na kesho yake aliondoka saa ngapi."


"Sawa, ila kifupi tu ni kwamba alifika mchana na aliondoka kesho yake jioni."

"Nakushukuru sana mpenzi, najua unakaribia kufika nyumbani, nikuache maana nasikia mumeo ana wivu sana." Maria aliangua kicheko cha umbeya.

"Hata mwenyewe una wivu." Akajibu.

"Niwe na wivu wakati huyo mume nimekupa mwenyewe."

"Hata kama umenipa, unadhani wivu huwa unaondoka kwenye moyo wa binadamu. Unaweza ukampa mtu kitu halafu ukamnyang'anya." Akajibu Maria na kusababisha kicheko kutoka kwa Eddy. Baada ya utani mwingine wa hapa na pale, wakaagana.




**"Enhee, niambie maana wewe naye inshu zako husomeki."**

**************************************

"Niambie bwana Rashid."

"Safi tu, za huko Dar es Salaam."

"Huku mara jua, mara mvua, ili mradi tu tupo katikati."

"Enhee, niambie maana wewe naye inshu zako husomeki."

"Yale yale tu, kuna kitu naomba unisaidie kidogo."

"Kitu gani hicho?"

"Nataka uniambie, kuna baadhi ya watumishi wa serikali hapo Dodoma mwanzoni mwa Desemba hivi walipata safari?"

Sekunde chache zilipita, halafu ni kama mtu aliyeshtuka hivi.

"Ahaa, ndiyo bwana Eddy, kuna Idara moja ya Maliasili ilikwenda Mwanza kwa semina ya siku tatu."

"Okay, walitumia usafiri gani kutoka hapo?"

"Walitumia basi. Mabasi mawili yaliyokodishwa na serikali ndiyo yaliyowapeleka huko."

"Mabasi hayo yalikwenda na hayakurudi tena?"

"Yalikwenda na kuwarudisha, baada ya siku nne au tano hivi."

"Wote walirejea?"

"Sina uhakika sana, lakini nadhani kuna watu walishukia njiani, nadhani wengine walibaki kidogo ili kumwagilia moyo, unajua tena, lakini hakupitisha siku mbili, kesho yake wakawa wamerudi."

"Okay, maana nimepata taarifa za ubadhirifu hapa wa fedha, sasa tunataka kuhakikisha kama ni kweli au la." Eddy akaongopa.

Eddy huwa na watu wake wa karibu ambao huwatumia kwenye kazi zake, lakini amekuwa wakiwatumia kupata taarifa sahihi, lakini hawapi kwa undani kabisa ni nini anachotaka kukifanya. Anaweza kuwapa kazi ya kumfuatilia mtu fulani au kitu fulani ili atumie mrejesho, lakini watu hawajui huyo mtu amefanya nini na sababu gani.

Rashid ni mmoja kati ya rafiki zake na watu wake ambao huwatumia sana. Ni mfanyakazi ya serikali ambaye yupo Dodoma kwa miaka miwili sasa.

Kile alichokuwa akikidhani, au kukifikiria kilianza kuonyesha mafanikio. Moja maelezo aliyoyapata kwa mjomba wa Tessy, alivutiwa na majina kadhaa aliyoyaulizia kiujanja. Akaanza kuyafanyia kazi. Akawa na wasiwasi na jina la mtu mmoja hivi. Alichofanya ni kuchunguza nyendo zake. Ndiyo akampa kazi Maria, mfanyakazi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Kambarage Nyerere.

Aliyemshuku ni huyu mfanyakazi wa Maliasili. Akapata taarifa zake kuwa anafanya kazi Dodoma, lakini mara kwa mara huja Dar es Salaam.

Safari zake zote alizotumia ndege ni kutoka Dar kwenda Dodoma kikazi na kurejea. Ni mara moja tu alitoka Mwanza kwa ndege kuja Dar na kesho yake akaenda Dodoma. Sasa kwa mujibu wa Rashid ni kwamba alikuwepo kwenye semina iliyoandaliwa kwa watumishi wa Maliasili. "Walitoka Dodoma kwa basi na walirudi kwa basi. Lakini huyu jamaa alipanda ndege na kurudi Dar, akiwaacha wenzake wakipumzika siku moja baada ya siku tatu za semina. Akaja kwa siku moja tu, kesho yake akaondoka kwenda Dodoma, siku ambayo wenzake nao walikuwa wanarejea. Kwa bahati mbaya sana, siku hii ambayo anatua mchana Dar, ndiyo siku ambayo mjomba wa marehemu Tessy anasema hakurejea nyumbani na maiti kuonekana siku tatu baadaye." Eddy alijisemea mwenyewe.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# TAIFA STARS YAIKAMIA NIGER

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya taifa 'Taifa Stars' kinaendelea na maandalizi ya mchezo wa kufuzu fainali ya AFCON huku wachezaji wakipania kupata ushindi kwenye mchezo huo wa kesho.

Timu hiyo chini ya Kocha Mkuu, Adel Amrouche imeanza maandalizi kuelekea mchezo huo huku baadhi ya wachezaji wakiweka wazi umuhimu wa mchezo huo wa kesho.

**Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa Shirikisho la Mpira wa miguu Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo alisema wachezaji wote walioitwa katika kikosi cha Stars wako kambini wanaendelea na maandalizi ya mchezo huo na wamepania kupata ushindi.**

"Wachezaji wanafahamu umuhimu wa mchezo wa kesho (leo) kama TFF tunafanya kila kitu kuona mambo yanaenda sawa," alisema Ndimbo na kuendelea,

"Ni lazima mechi ya kesho tupate matokeo yaliyo chanya, wachezaji wanaitaka hii mechi, maandalizi yanafanyika kwa ajili ya kupata matokeo mazuri kwa sababu ushindi katika mchezo huu utatuweka kwenye mazingira mazuri ya kufuzu", alisema Ndimbo.

Aidha alisema kuwa wapinzani wao wamewasili nchini jana (juzi) kwa ajili ya mchezo huo muhimu.

Ushindi kwenye mchezo huo wa kesho utaifanya Stars kufikisha pointi saba na kuwapa uhakika wa kufuzu endapo Uganda ambayo ipo chini ya Stars itapoteza mchezo wake dhidi ya Algeria.

Stars ipo kundi F linaloongozwa na Algeria wakiwa na alama 12, Tanzania ikiwa na pointi 4 sawa na Uganda na Niger inashika nafasi ya mwisho ikiwa na pointi moja.



Vijana wakicheza mpira wa Kikapu katika viwanja vya Kituo cha kukuza vipaji cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kikwete kushiriki JKT Marathon*

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Mrisho Kikwete anatarajia kushiriki mashindano ya Kilomita tano ya mbio za JKT Marathon zilizopangwa kufanyika Juni 25 katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Mbio hizo ambazo zitajumuisha wanariadha kutoka sehemu mbalimbali pamoja na wananchi kwa ujumla zitaanzia katika uwanja wa Jamhuri kuelekea barabara ya Iringa, St John na kurejea katika uwanja wa Jamhuri.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa uzinduzi wa vifaa vya michezo ambavyo vitatumika katika mashindano hayo, Mkurugenzi wa Elimu Utamaduni na Michezo wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT),Kanali Erasmus Bwegoge alisema lengo la mashindano hayo ya riadha ni pamoja na kuadhimisha miaka 60 ya JKT toka jeshi hilo lianzishwe.

Alifafanua zaidi kuwa maandalizi ya mashindano hayo ya riadha tayari yamekamilika huku akisisitiza wananchi pamoja na wadau wa michezo kujitokeza kushiriki mashindano hayo.

"Maandalizi ya mashindano hayo tayari yamekamilika,tunaomba watu waendelee kujiandikisha kushiriki, mashindano haya yatasaidia sana kuimarisha afya za washiriki," alisema Kanali Bwegoge.

Mbali na Kilomita tano pia alisema kutakuwa na mbio za Kilomita 10 kwa wanawake na wanaume na Kilomita 21.1 kwa wanawake na wanaume ambazo washindi watakabidhiwa zawadi ya medali na fedha taslimu.

"Msindi wa Kilomita tano atapata medali huku upande wa Kilomita 10 mshindi wa kwanza atapata sh 500,000 na medali, mshindi wa pili ataibuka na kitita cha sh 300,000 na watatu atapata sh 200,000, wanne ataibuka na sh 150,000 huku watano ataondoka na sh 100,000 na mshindi wa sita hadi wa 10 watapata sh 50,000" alisema Kanali Bwegoge.

Aidha alisema kwa upande wa Kilomita 21.1 mshindi wa kwanza atapata Shilingi milioni moja, mshindi wa pili atapata Sh 800,000 na watatu atapata sh 600,000.

Mshindi wa nne katika mbio hizo ataondoka na sh 400,000,watano atapata sh 200,000 na mshindi wa sita hadi 10 watapata sh 100,000.

Alisema washindi katika mbio zote watakabidhiwa zawadi za medali na kusisitiza raia wajitokeze kwa wingi kushiriki mashindano hayo.

Pia alisema vifaa kwa ajili ya ushiriki vitaanza kutolewa leo mpaka Juni 24 na washiriki waliojiandikisha waende kwenye maeneo yao kuvichukua.

## Mashindano U-20 kuanza Juni 21

**Na Abdallah Mataka**

MASHINDANO ya vijana chini ya umri wa miaka 20 yamepangwa kuanza kutimua vumbi Juni 21 kwenye uwanja wa Azam complex jijini Dar es Salaam.

Ligi hiyo inashirikisha timu za vijana kutoka katika klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mtibwa Sugar ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo na wamepangwa kwenye kundi A pamoja na timu za Ruvu Shooting ya Pwani, Mbeya City (Mbeya) na Namungo FC ya Ruangwa Mkoani Lindi.

Kundi B linaundwa na Yanga SC ya (Dar es Salaam), Polisi Tanzania( Kilimanjaro), Dodoma Jiji ya (Dodoma) na Tanzania Prisons ya (Mbeya), wakati Kundi C linaundwa na Coastal Union ya (Tanga), Geita Gold ya (Geita), Singida Fountain Gate FC ya (Singida) na KMC ya Kinondoni Jijini (Dar es Salaam).

Kundi D kwenye mashindano hayo linaundwa na Simba SC na Azam FC ,(Dar es Salaam) ,Ihefu SC (Mbeya) na Kagera Sugar ya Bukoba.

## Lukula apata shavu Uganda

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa timu ya Wanawake Simba Queens, Charles Lukula amepata ofa ya kuifundisha timu ya Taifa ya Wanawake ya Uganda The Crested'.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana kutoka Uganda Kocha huyo alisema baada ya kumaliza mkataba wake na Simba amepokea ofa nyingi hapa nchini na Uganda ikiwemo timu ya taifa ya wanawake ya Uganda.

"Tangu niondoke Tanzania nimepokea ofa nyingi baadhi zinatoka kwenye timu za Ligi Kuu za wanaume na wanawake pamoja na hii ya Uganda ninachoangalia ni maslahi yangu, naifikiria zaidi timu yangu ya taifa ya wanawake," alisema Lukula.

Kocha huyo alisema Wakala wake Mujibu Kasule anaendelea kufanya mazungumzo na klabu mbali mbali pamoja na timu hiyo ya taifa.

"Mimi siruhusiwi kuzungumza nazo, Wakala wangu ndio anafanya mazungumzo tukikamilisha mipango yote nitawafahamisha ninapo kwenda," alisema Lukula.

Aidha alisema anaushukuru Uongozi wa Klabu ya Simba kwa kumuamini na kumpa nafasi yakufundisha timu yao ya wanawake na amejifunza mengi.

Alisema Ligi Kuu ya Wanawake ya Tanzania ina ushindani mkubwa ukilinganisha na nchi nyigine hususaani za Afrika masharikі ambazo zinapaswa kujifunza kwao.

"Soka la Tanzania kwa wanawake imepiga hatua kubwa sana, timu nyingi zina wachezaji a kimataifa na wanaleta ushindani kwa wachezaji wazawa, tanzania imepiga hatua kubwa sana ." alisema Lukula.

Aisha walisema wameukosa kutetea ubingwa wao msimu huu kutokana mapungufu kwa baadhi ya maene ikiwemo eneo la golikipa.

"Mimi ningepata ubingwa isipokuwa makipa wangu ndio wameniangusha na timu yangu ilikuwa imefanya vizuri kwenye michezo yake yote, ni jambo la kuliangalia ," alisema Lukula.

## ZISIKUPITE

**MAN NA KANE**
KLABU ya Manchester United wameachana na nia yao ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29 kutoka Tottenham Hotspur msimu huu wa joto kwa kuwa wanahisi ada hiyo itakuwa juu sana. (*Gardian*)

**BARELLA AWANIWA NEWCASTLE**

NEWCASTLE United inakaribia kukubali mkataba wa pauni milioni 50 na Inter Milan kwa kiungo wa kati wa Italia, Nicolo Barella mwenye umri wa miaka 26. (*Telegraph*)

**HAVERTZ ATAKIWA ARSENAL**

KLABU ya Arsenal inawania kumsajili Kai Havertz kutoka kwa wapinzani wao wa London Chelsea, ambao watahitaji pauni milioni 70 kwa fowadi huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 24. *(Guardian)*

**VLAHOVIC AWINDWA**

JUVENRUS Inataka angalau euro milioni 80 kwa Dusan Vlahovic, lakini Chelsea wamewaambia Waitaliano hao kwamba wanaweza kuchagua kati ya wachezaji watano katika makubaliano ya kubadilishana na mshambuliaji huyo wa Serbia mwenye umri wa miaka 23. *(Gazzetta dello Sport, via Football Italia*)

**JAMES HAONDOKI**

KLABU ya Manchester City itapinga ofa za mkopo kwa kiungo wa kati, James McAtee mwenye umri wa miaka 20, ambaye wanamtaka kwenye kikosi chao msimu ujao. (*Mail)*

**CAICEDO SOKONI**

CHELSEA iko tayari kufikia dau lolote ambalo Arsenal watawasilisha kwa Moises Caicedo wa Brighton, wakati Bayern Munich pia wanatazamia kumnunua kiungo huyo wa Ecuador mwenye umri wa miaka 21. (*Football Insider)*

**RAYA SAFI**

GOLIKIPA wa Brentford na Hispania, David Raya mwenye umri wa miaka 27, amekubaliana maslahi binafsi kuhusu kuhamia Tottenham Hotspur. (*Fabrizio Romano*)

**FOREST YAKATAA**

KLABU ya Nottingham Forest imekataa dau la rekodi la klabu la pauni milioni 30 kwa mshambuliaji wa Wales, Brennan Johnson mwenye umri wa miaka 22 kutoka Brentford. (*Sky Sports*)

**TOURE AGOMBEWA**

KLABU za Burnley na Bournemouth zinaongoza mbio za kumsajili mshambuliaji wa Mali, El Bilal Toure mwenye umri wa miaka 21 kutoka Almeria msimu huu wa joto. (*Football Insider)*

**DOUE AWANIWA**

KLABU ya Newcastle imekuwa ikiwasiliana na wawakilishi wa kiungo wa kati wa Rennes, Mfaransa Desire Doue, ambaye alitimiza umri wa miaka 18 mwezi huu na amewavutia Barcelona na Paris St-Germain. (*ESPN*)

**SEVILLA NA MONCHI**
KLABU ya Aston Villa imekubaliana na Monchi kuondoka Sevilla na kuwa mkurugenzi wa michezo wa Villa, ambapo ataungana na kocha Unai Emery. (*Football Insider*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO APATA MCHONGO SAUDIA

**ROME,** Italia

JOSE Mourinho anaripotiwa kuwa kwenye mipango ya kubamba dili la pesa nyingi kutoka Saudi Arabia.

Kocha huyo Mreno amebakiza miezi 12 tu katika mkataba wake wa sasa huko katika klabu ya AS Roma.

**Kumekuwa na uvumi kwamba anafikiria mpango wa kuondoka kwenye majira haya ya kiangazi huko Ulaya baada ya AS Roma kushindwa kukamatia tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mis imu yote miwili aliyokuwa akiinoa timu hiyo.**

Kwa mujibu wa Foot Mercato, klabu ya Al-Hilal imemworodhesha Mourinho kuwa chaguo lao la kwanza kwenye msako wa kocha mpya na kwamba wameandaa ofa nono kabisa ili akapige kazi huko Mashariki ya Kati.

**●●● Dili likifanikiwa kuwa miongoni mwa makocha wanaolipwa pesa nyingi duniani...**

Na kinachoelezwa ni kwamba Mourinho mwenye umri wa miaka 60, atapewa mkwanja mrefu wa kusajili.

Roma wanataka kumbakiza Mourinho, lakini wamefungua milango ya kuachana na kocha huyo na kutafuta mwingine wa kuja kuchukua mikoba yake. Ligi Kuu Saudi Arabia, Saudi Pro League ipo bize kwa sasa kuvuta mastaa wenye majina makubwa kwenye soka kwenda kwenye ligi hiyo.

Cristiano Ronaldo alifungua milango kwa kujiunga na Al-Nassr, wakati fowadi mwingine wa zamani wa Real Madrid, Karim Benzema naye amejiunga na Al-Ittihad. Kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante yupo kwenye hatua za mwisho kujiunga na Al-Ittihad huku Al-Ahli wakihitaji pia saini ya mkali wa Manchester City, Riyad Mahrez.

Taarifa nyingine za kutoka Saudi Arabia, zinadai kwamba Al-Hilal inayomtaka Mourinho, inamtaka pia Neymar.

# Ferdinand: Ununuzi wa United umekaribia

**MANCHESTER,** Englad


GWIJI na beki wa zamani wa klabu ya Manchester United na timu ya taifa ya England, Rio Ferdinand amesema klabu ya Manchester United ipo kwenye hatua za mwisho kununuliwa na wamiliki wa Qatar.

Ferdinand ameyazungumza hayo akisema kutoka katoka vyanzo vyake vya kuaminika ununuzi wa klabu ya Man United upo karibuni na wanunuzi watakua kutoka Qatar ambao wamekua wakihusishwa kuinunua klabu hiyo wakiongozwa na Sheikh Jassim.

Beki huyo wa zamani wa klabu hiyo anasema anaomba wamiliki wa klabu hiyo familia ya Glazers wahakikishe wanakamilishe mchakato huo haraka ili klabu hiyo iweze kufanya usajili vizuri katika dirisha hili kubwa ambalo limefunguliwa jana.

Klabu ya Man United iliwekwa sokoni kuanzia mwaka jana mwishoni na wamiliki wa klabu hiyo familia ya Glazers ambapo mchakato wa kuinunua klabu umedumu kwa takribani miezi sita, huku taarifa zikieleza Glazers ndio wanakwamisha dili hilo kukamilika.

Ferdinand pamoja na magwiji wengine wa klabu hiyo wamekua wakitamani Glazers waiachie timu hiyo kwani anaona ni kama wamefeli kuiongoza klabu hiyo siku za hivi karibuni na klabu hiyo imekua ikiporomoka siku hadi siku kiwanjani.






# BELLIGHAM, MAGUIRE, SANCHO GHALI ZAIDI ENGLAND

**LONDON,** England

HAKUNA mchezaji mzuri anayenunuliwa kwa bei rahisi na hii imethibitishwa na Real Madrid baada ya kuonyesha jeuri ya fedha kufuatia usajili wao uliovunja rekodi England baada ya kumsajili kiungo, Jude Bellingham kutoka Borussia Dortmund.

Kiungo huyo wa kimataifa wa England sasa anaweka rekodi ya kuwa mwanasoka ghali zaidi wa Uingereza kufuatia uhamisho wake wa kutoka Dortmund kutua Santiago Bernabeu kugharimu Pauni 115 milioni.

Aidha mbali na Bellingham, mchezaji mwengine wa bei kubwa England ni Jack Grealishi wa Machester City.

Manchester City ilimnunua kiungo huyo kwa ada ya uhamisho wa Pauni 100 milioni akitokea Aston Villa, katika usajili wa dirisha la kiangazi.

Ingawa alichukua muda mrefu kufiti kikosini msimu wake wa kwanza, sasa kiungo huyo amekuwa mchezaji mwenye mchango mkubwa.

Msimu uliopita alicheza mechi 50 na akasaidia Man City kubeba mataji matatu na kufidia pesa aliyonunuliwa. Grealish alikuwa gumzo mtandaoni kutokana na shangwe lake ubingwa kwa muda wa siku nne.

Mchezaji mwingine wa bei ni beki wa kati wa Machester United, Harry Maguire, beki huyu alijiunga na Manchester United tangu mwaka 2019 kwa kitita cha Pauni 85 milioni akitokea Leicester City. Maguire amechezea Man United mechi 157, lakini amepitia kipindi kigumu. Beki huyu hakutoboa chini ya kocha Erik ten Hag na taarifa zinaripoti huenda akaondoka kutokana na kutopewa muda wa mwingi wa kucheza .

**Sancho**



Sancho alisajiliwa na Manchester United akitokea Borussia Dortmund mashabiki walikuwa na matarajio makubwa kutoka kwake. Kama ilivyokuwa Maguire, winga huyu hakuwa na misimu mizuri. Hata hivyo kocha Erik ten Hag bado anaamini staa wake huyo ana kipaji cha kucheza soka. Msimu wake wa kwanza Sancho alifunga mabao nane katika mechi 38 alizocheza. Kiwango chake kilishuka kutokana na majeraha na maradhi yaliyokuwa yakimsumbua.



**White**

White alijiunga na Arsenal mwaka 2021 kwa ada ya ujamisho wa Pauni 50 milioni akitokea Brighton. Ingawa mashabiki waliponda kiwango cha pesa aliyonunuliwa, lakini beki huyo amekuwa tegemeo kikosini kinachonolewa na Mikel Arteta.

Winga huyo wa zamani wa Liverpool alijiunga na Manchester City kwa Pauni 49 milioni mwaka 2015. Alifunga mabao 131 katika mechi 339 alizocheza Etihad kabla ya kutimkia Chelsea. Msimu uliopita alicheza mechi 38 katika mashindano yote akiwa na uzi wa Chelsea.

# Immobile: Hispania haikuwa na nafasi nyingi

**ROME,** Italia

CIRO Immobile ameasisitiza kuwa Hispania haikutengeneza nafasi nyingi zaidi kuliko Italia na 'sare ilikuwa ya haki' katika nusu fainali ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, lakini iliishia kwa kupoteza 2-1.

Immobile alifunga mkwaju wa penalti na kusawazisha matokeo baada ya mwanzo mbaya, ambao ulimfanya Leonardo Bonucci kumiliki mpira kwa bao la kwanza la Yeremy Pino dakika ya tatu.

Katika dakika za mwisho za mechi hiyo, bao la Rodri lilimruhusu mchezaji wa akiba Joselu kunyakua ushindi kwa Hispania.

Immobile amesema; "Tulipigana hadi mwisho, kwa bahati mbaya hii ricochet mara mbili kwenye goli ilitua kwenye miguu ya washambuliaji wao. Huu ni mpira wa miguu, tulikuwa tunacheza vizuri, lakini mambo haya yanatokea.

"Siku zote ni ngumu dhidi ya Uhispania, wanashika mpira na kukuchosha, lakini hawakutengeneza nafasi nyingi kwa kweli. Kwa upande wa nafasi za kufunga, nadhani sare ilikuwa ya haki," alisema mchezaji huyo.

Italia sasa itamenyana na wenyeji Uholanzi Jumapili alasiri kuwania nafasi ya tatu katika Ligi ya Mataifa ya Uefa, huku baadaye jioni hiyo Uhispania na Croatia zikimenyana kuwania kombe hilo.

Ni mara ya pili kwa Azzurri kufika Fainali ya Nne ya Ligi ya Mataifa na kushindwa na Uhispania katika nusu fainali.

Nazionale pia wako chini ya shinikizo baada ya kuanza vibaya kwa kampeni ya kufuzu kwa Mashindano ya Uropa ya 2024.



HABARI MICHEZO

# 'THANK YOU' ZA WACHEZAJI SIMBA KUANZA JUMATATU

Na Adam Fungamwango

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema kuanzia Jumatatu utaanza kutangaza majina ya wachezaji ambao hawatokuwa nao msimu ujao.

Klabu za Simba, Yanga na Azam zimekuwa na utaratibu wa kumalizana na wachezaji wao na kisha kuposti kwenye kurasa za mitandao yao na neno "Thank You' kumaanisha kushukuru kile wachezaji wao walichokifanya kwa muda wote wakiwa kwenye timu hizo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema tayari Bodi ya Wakurugenzi imeshamaliza kupitia ripoti na mapendekezo ya Kocha Mkuu, Roberto Oliveira, hivyo kwa sasa wanachofanya ni kuzungumza na wachezaji ambao wataachwa, kabla ya kuwatangaza.

"Tulikuwa tunamalizia hapa kupitia ripoti ya mwalimu, Bodi ya Wakurugenzi imeshapitia ripoti ya mwalimu, imeshapitia mapendekezo yake sasa tupo kwenye mazungumzo na wachezaji husika ambao tunakusudia kuachana nao, kwa sababu wapo wengine wana mikataba hatuwezi kuwaacha tu kihuni huni, ni lazima ukae uzungumze nao kila mmoja aridhike ili kuepusha kesi baadaye kwa hiyo hadi kufika Jumatatu, tuatanza kuacha majina ya wachezaji ambao tumeshamalizana nao," alisema Ahmed.

Akizungumzia kuachana na baadhi ya watu wa benchi la ufundi, alisema hiyo inatokana na mpango wao wa kukifanyia maboresho kikosi chao na wanaanzia kwenye benchi la ufundi.

Mpaka sasa tayari Simba wameaachwa kocha wa magolikipa, Chlouha Zakaria, kocha wa viungo Kelvin Mandla na mtaalam wa viungo.

Pia Simba jana imetangaza kuachana na kocha wa timu ya wanawake Charles Lukula raia wa Uganda.

"Ni kweli tunawapa mkono wa kwa heri wale ambao hatutakuwa nao kwa msimu ujao, nia ni kuitengeneza Simba imara, kila kitu kinaanzia kwenye benchi la ufundi kwa hiyo tumeamua kuwaondoa hawa ambao tuliokuwa nao, pamoja na na ukweli kuwa wamefanya kazi kubwa ya kuisaidia Simba misimu iliyopita huko nyuma, lakini sasa tunahitaji kuelekea sehemu kubwa zaidi, tuna maono na malengo makubwa kwa hiyo ni lazima utafute watu wa kukaa kwenye hayo malengo, tunatafuta watu ambao tunaamini watakwenda kuisaidia Simba kwenda juu zaidi," alisema Ahmed.

Aidha, alisema hayo yote ni maboresho ya kuirejesha Simba kwenye ramani na ufalme wake kwa sababu wamekaa misimu miwili kwa timu ya wanaume bila taji lolote.

Ahmed alisema makocha Robertinho na Juma Mgunda wataendelea kuwa sehemu ya benchi la ufundi la timu hiyo.



Wachezaji wa timu ya walemavu ya Sauti Pala Sports, Adam Hassan kulia na, Sajati Mtupa, wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi jana kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ibenge atajwa kumrithi Nabi

INATOKA UK 24

alisema Kamwe.

Alisema kwa sasa wapo kwenye mchakato unaofanywa taratibu na kwa umakini mkubwa ili kumpata kocha ambaye ataendeleza pale alipoishia Nabi.

"Kwa hiyo, niwaambie wanachama na mashabiki wanaoitakia heri Yanga, mchakato unakwenda taratibu kwa utulivu na kwa umakini mkubwa ili kutafuta kocha ambaye ataanzia hapa ambapo tumefikia tusirudi nyuma, na mbele ninaposema ni kuendeleza utawala wetu kwenye makombe ya ndani na kumalizia kazi iliyofanywa na Nabi ya kutwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika kwa sababu yeye alifika Fainali," alisema Kamwe.

Aidha alisema wakati yanga ikiendelea na mchakato wa kumsaka mrithio wa Nabi, uongozi upo kwenye mazungumzo nay a kuwaongezea mkataba makocha wasaidizi Cedric Kaze raia wa Burundi na kocha wa viungo, Mtunisia, Helmy Gueldich.

Rais wa Klabu hiyo, Injinia Hersi amesema mazungumzo na walimu hao ya kutaka kuwapa mikataba mipya yanaendelea na watakachoafikiana watawaeleza wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

Zipo taarifa kuwa Kaze anatakiwa kwa udi na uvumba na klabu za Singida Fountaine Gate na Geita Gold kwa ajili ya kuvinoa vikosi vyao.

Kaze, Gueldich na kocha wa makipa Mbrazili, Milton Nienov wote wamemaliza mikataba yao ndani ya Yanga , huku kukiwa na taarifa za Nabi kuwahitaji kwenye klabu anayokwenda ambayo inatajwa kuwa ni Kaizer Chiefs.

## Azam U 17 yaziburuza Simba, Yanga

Na Adam Fungamwango

TIMU ya vijana ya Azam chini ya miaka 17 imeendelea kufanya vema na kuongoza Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) inayoendelea kwenye Viwanja wa vya Kituo cha Ufundi, TFF, Kigamboni Dar es Salaam.

Mpaka kufikia raundi ya sita, Azam inaongoza ligi hiyo ikiwa imefikisha pointi 18, ikicheza mechi sita na kushinda zote, ikifunga mabao 19 na kufungwa moja tu, ikifuatiwa na Ihefu SC ambayo imeonekana kuja juu kila raundi zinapozidi kuongezeka, ikifikisha pointi 16, kwa kucheza mechi sita na kushinda tano ikitoa sare moja.

Yanga ambayo iliongoza ligi hiyo mpaka kufikia raundi ya nne, imeteremshwa hadi nafasi ya tatu ikiwa na pointi 14, ikicheza mechi sita, ikishinda nne na sare mbili.

Singida Big Stars ipo kwenye nafasi ya nne kwa pointi 13, na nafasi ya tano inashikiliwa na Simba ambayo ina pointi 12, ikicheza mechi sita na kushinda tatu huku ikitoka sare mechi tatu.

Mbeya Kwanza inashika nafasi ya sita kwa pointi 11, Ruvu Shooting nafasi ya saba, pointi 10, nafasi ya nane inakwenda kwa Karume Youth Centre yenye pointi nane, JKT Tanzania ionashika nafasi ya tisa ikiwa na pointi saba, African Sports inashika nafasi ya 10 ikiwa na pointi saba.

Transit Camp ipo kwenye nafasi ya 11 na pointi zake sita, KMC ipo nafasi ya 12 ikiwa na pointi tano, African Lyon inakamata nafasi ya 13 ikiwa na pointi tatu, Pan African ina pointi tatu na inashika nafasi ya 14.

Nafasi ya 15 inakamatwa na JKU Academy yenye pointi mbili, na timu inayoshika mkia ni Green Warriors ambao imepoteza mechi zake zote sita, ikiwa haina pointi, ikifunga mabao mawili tu.

## Sandaland yashusha neema Simba

INATOKA UK 24

mahitaji ya mashabiki wa Simba na kampuni yake imejipanga vyema kuwaondolea 'kiu' ya kukosa jezi za klabu yao wanayoipenda kwa wakati.

"Tumekuja kufanya mapinduzi katika soko la vifaa vya michezo, tunaahidi Simba itakuwa moja ya klabu za Afrika zinazovaa jezi zenye ubora mkubwa na hadhi inayofanana na ukubwa na heshima ya klabu," alisema mdhamini huyo.

Msimu uliopita Simba iliingia mkataba na Vunjabei, lakini kampuni hiyo ilipata changamoto ya kuchelewesha jezi na kupelekea mashabiki wengi kukosa jezi mpya kama ilivyotarajiwa.

Simba iliyomaliza msimu uliopita katika nafasi ya pili, msimu ujao inatarajia pia kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la FA.

Michezo

Nipashe

Jumamosi Juni 17, 2023



UK. 21

Mourinho apata mchongo Saudia



Wachezaji wa timu ya taifa 'Taifa Stars' wakiwa kwenye mazoezi kujiandaa na mchezo wao wa kesho dhidi ya Niger wa kufuzu fainali za AFCON mwakani. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Kocha Ibenge atajwa kumrithi Nabi Yanga

## ●●● Uongozi wapambana kuwabakisha Kaze, Gueldich...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Yanga wapo 'kazini' kusaka Kocha Mkuu wa timu hiyo baada ya kuondoka kwa Mtunisia, Nasreddine Nabi huku Mkongomani Florent Ibenge akipewa nafasi kubwa kutua kikosini hapo.

**Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema mbali na kocha huyo, makocha wengine wanao tajwa kuwa na asilimia kubwa ya kuvaa viatu vya Nabi ni Juan Carlos Garrrido kutoka Hispania, Watunisia Fouuzi Benzarti, Nabil Maaloul, na Julien Chevalier kutoka Ufaransa.**

Mmoja wa viongozi wa Yanga aliiambia Nipashe kuwa Ibenge ni miongoni mwa makocha ambao Uongozi wa klabu hiyo unataka kuwa naye msimu ujao.

"Nabi ameondoka kwa amani kabisa, lakini tunataka kupata kocha ambaye atatuvusha kutoka hapa tulipo, kutoka pale Nabi alipotufikisha, tayari uongozi umemfikiria Ibenge na kama mazungumzo yataenda vizuri ataungana na sisi," alisema kiongozi huyo.

Aidha, alisema wapo makocha wengine ambao klabu inafikiria kuwachukua lakini kwa sasa kipaumbele chao cha kwanza ni Mkongomani huyo.

"Kwa sasa hao ndio makocha ambao Uongozi unaangalia uwezekano wa mmoja wapo kuja Yanga, mambo yakikaa sawa mmoja wapo atatangazwa kuwa kocha wa Yanga," alisema kiongozi huyo.

Nipashe ilimtafuta kocha Ibenge anayefundisha klabu ya Al Hilal ya Sudan amnaye hakukataa wala kukubali kuwa yupokenye mazungumzo na Yanga.

"Bado Nina mkataba na Al Hilal japo kuwa hatuchezi ligi kutokana na hali halisi ya machafuko ndani ya Sudan ambayo yameathiri ligi kuu, kuhusu Yanga siwezi kusema kitu kwa sasa kwa sababu zipo klabu nyingi zinahitaji nifanye nazo kazi," alisema Ibenge.

Aidha, alisema kama kutakuwa na lolote Watanzania watajua lakini kwa sasa yeye bado ni mwajiriwa wa Al Hilal.

Aidha, Afisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe alisema tangu kuandoka kwa Nabi, wamepokea CV nyingi za makocha kutoka sehemu mbalimbali zikiomba nafasi ya kufundisha timu hiyo.

"Tangu tulipotoa taarifa za kuachana na Nabi hadi leo hii, CV nyingi sana zimetumwa kutoka sehemu mbalimbali Afrika na nje ya Afrika, nazungumzia makocha wakubwa, uzuri ni kwamba klabu yetu kwa sasa ni kubwa na huu wingi wa makocha kutaka kufanya kazi Yanga unathibitisha kwa vitendo kazi nzuri ya viongozi kuitangaza klabu yetu, Yanga kwa saa imeanza kuonekana kwa makocha wakubwa duniani kutamani kufanya nayo kazi,"

INAENDELEA UK 23

# Sandaland yashusha neema Simba SC

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba imeingia mkataba na Kampuni ya Sandaland Fashion Wear kwa ajili ya kupatiwa jezi na vifaa mbalimbali vya michezo wenye thamani ya Sh.bilioni nne, imeelezwa jana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema mkataba huo na Sandaland Fashion Wear ni wa miaka miwili na kila mwaka klabu itapokea vifaa vyenye thamani ya Sh.bilioni mbili.

Ahmed alisema klabu imefikia uamuzi wa kuingilia makubaliano na kampuni hiyo baada ya kujiridhisha na namna itakavyotekeleza makubaliano kwa ajili ya maslahi ya Simba.

"Tunapenda kuchukua nafasi hii kumtambulisha rasmi mdhamini wetu mpya katika masuala ya jezi na vifaa, na si mwingine ni Sandaland The Only One, tunaamini kila kitu kitakwenda vyema baada ya kujiridhisha," alisema Ahmed.

Mkurugenzi wa Sandaland Fashion Wear, Yusuf Yenga, alisema kampuni yake imefarijika kupata nafasi hii na inaahidi itaitendea haki nafasi ambayo wameipata ndani ya klabu ya Simba.

Yenga alisema tayari jezi zimeshatengenezwa na zitaingia rasmi sokoni kabla ya Tamasha la Simba Day na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa mwaka 2023/2024 haujaanza.

Aliongeza jezi na vifaa vitakavyoletwa na kampuni yake vitakuwa na ubora wa hali ya juu na anatarajia vitapendwa na mashabiki na wadau wote wa michezo wa ndani na nje ya Tanzania.

"Napenda niwaambie wanachama, mashabiki na wanamichezo kampuni yangu imejipanga imara katika kufanikisha upatikanaji wa jezi na vifaa vyote muhimu kwa wakati, jezi zitakuwa nyingi sokoni na za kiwango cha juu, nawahakikishieni," alisema Yenga.

Aliongeza anafahamu vyema

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042